# TATHMINI YA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI KAUNTI YA MURANG'A KENYA

**NA**

**MUIGA HARRISON GATUTHU**

**C50/OL/CTY/25923/2014**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI, 2021**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

Sahihi________________________tarehe_______________

MUIGA HARRISON GATUTHU

C5O/OL/CTY/25923/2014

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi

Sahihi_______________________tarehe ___________________

DKT. JACKTONE ONYANGO

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

IDARA YA KISWAHILI

Sahihi______________________tarehe___________________

DKT. STEPHEN KAMAU

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

IDARA YA KISWAHILI

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa mke wangu Joyce Njoki, watoto wetu Maxmillian Muiga, Ruth Kellen Nyokabi na Jane Wairimu, wazazi wangu Joseph Muiga na Kellen Nyokabi. Asanteni kwa stahamala yenu. Mmekuwa motisha kwangu. Kwa marehemu nyanya yangu, Margret Njeri, heko, ulipanda mbegu ya elimu kwangu na sasa imenawiri. Nyote mmechangia ufanisi huu kwa kiasi kikubwa. Tumeshinda pamoja.

## SHUKRANI

Kwanza namshukuru mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake kwangu hadi kufikia kiwango hiki cha uzamili kimiujiza tu. Siwezi kueleza. Ni Baraka.

Shukran kwa wasimamizi wangu Daktari Jacktone onyango na Daktari Stephen Kamau, kwa ushauri na maelekezo yenu katika kila hatua ya kazi hii. Mmenitia moyo wa kuendelea bila kutamauka. Nawavulia kofia.

Aidha, nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mlinitia shime kila wakati. Asanteni.

Mwisho nawashukuru wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu wakiongozwa na baadhi ya walimu wa Kiswahili kaunti ya Murang'a waliofanikisha ukusanyaji data katika utafiti huu. Shukrani na Mungu awabariki.

## IKISIRI

Mahitaji ya silabasi mpya ya Kiswahili (2006) kwa shule za upili hupendekeza ufunzaji wa mada za sauti na matamshi. Suala la matamshi ya lugha, linahusika na matawi ya fonetiki na fonolojia. Matawi ya fonetiki na fonolojia ya lugha yoyote ile hujenga msingi wa matawi mengine ya lugha husika. Watahiniwa wa K.C.S.E. wamekuwa wakiripoti matokeo mabaya katika karatasi ya lugha 102/2 mwaka baada ya mwaka. Mojawapo ya vipengele vinavyotahiniwa katika karatasi hii ni mada za sauti na matamshi bora. Aidha, ilikisiwa kuwa mojawapo ya sababu za wanafunzi wengi kutojieleza vizuri kwa lugha sanifu ya Kiswahili ni kukosa msingi bora wa fonetiki na fonolojia. Hivyo basi kulikuwa na haja kubwa ya kutathmini kwa undani hali halisi ya ufunzaji wa matamshi katika shule za upili nchini Kenya. Malengo ya utafiti yalikuwa kutathmini yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili, kubainisha mbinu za ufunzaji sauti na matamshi katika shule za upili na kuchunguza changamoto katika ufunzaji wa mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya fonolojia zalishi iliyoasisiwa na Chomsky na Halle (1968). Nadharia hii imebainisha sauti za lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia kipengele cha uwilisifa. Vile vile, nadharia ya utabia iliyoasisiwa na Skinner (1957) ilitumika kushughulikia suala la ufundishaji wa matamshi ya Kiswahili. Utafiti wa maktabani na wa nyanjani ulizalisha data kuhusu mbinu na changamoto za ufunzaji sauti na matamshi katika shule za upili. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi ambapo shule kumi na nne; mbilimbili katika kila kaunti ndogo zilizoko katika kaunti ya Murang’a ziliteuliwa. Wanafunzi sita na walimu wawili wawili kwa kila shule waliteuliwa kuunda sampuli ya watafitiwa 112. Mbinu za hojaji, na mazoezi kwa wanafunzi zilitumiwa kukusanya data. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo, kwa njia ya majedwali na michoro duara. Uchanganuzi wa kitakwimu ulifanyika kwa kutumia mbinu ya tarakilishi ya uchanganuzi tarakimu sayansi za kijamii. Utafiti huu uligundua kuwa, ufunzaji matamshi ya Kiswahili umetiliwa uzito zaidi katika vidato vya chini (kidato cha kwanza na kidato cha pili) na kupuuzwa katika vidato vya juu (kidato cha tatu na kidato cha nne). Aidha, uzoefu wa kutosha wa mada za matamshi ya Kiswahili haukubainika katika silabasi ya Kiswahili kutoka kidato kimoja hadi kingine. Utafiti huu vile vile ulibaini changamoto mbalimbali katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili kama vile, mielekeo hasi ya walimu na wanafunzi kuhusu mada za matamshi ya Kiswahili, wanafunzi kuathiriwa na lugha zao za kwanza, ukosefu wa vifaa muhimu vya kufunzia matamshi kama vinasa sauti na athari za lugha ya sheng’ kwa wanafunzi. Utafiti huu ulihitimisha kwa kupendekeza marekebisho ya silabasi ya Kiswahili katika mada za matamshi ya Kiswahili ili kuwe na mwendelezo wa yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili kutoka kidato kimoja hadi kingine. Utafiti huu utawafaa wakuzaji mitaala kwani watabaini changamoto zinazokumba ufunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili na kufanya marekebisho yanayohitajika. Aidha walimu na wanafunzi, wahadhiri pamoja na vyombo vya utangazaji vitafaidika kwa njia za kuandaa wanafunzi na walimu wa lugha kuhusu mbinu mwafaka za ufunzaji sauti na matamshi ya Kiswahili.

## ABSTRACT

Sounds and pronunciations are linked with the linguistic branches of phonetics and phonology. Phonetics and phonology of any language builds the foundation of all other elements of language. As a result, the new Kiswahili secondary school syllabus (2006), recommends teaching of aspects of phonetics and phonology. K.C.S.E. candidates have been registering poor results in Kiswahili paper and especially in Kiswahili paper two (102/2) year after another. Sounds and pronunciation aspects are always tested in this particular paper. One of the major reasons why many students are not able to communicate in fluent Kiswahili language, is due to their poor acquisition of phonetic and phonology basics. Therefore, there was enough need of examining deeply the actual situation of learning and teaching of sounds and pronunciation in Kenyan secondary schools. Objectives of this study were to; examine the actual content taught in Kenyan secondary schools concerning Swahili sounds and pronunciation; to outline the various methods used in teaching and to find out the challenges in teaching sounds and pronunciation as well as giving the necessary recommendations. The study was guided by generative theory by Chomsky and Halle (1968). This theory analysed Kiswahili sounds using the aspects of binary character. Behavioural theory founded by Skinner (1957) assisted to analyse data on methodology of teaching Swahili sounds and pronunciation. The research was conducted in the library and in the field. In the library, literature review on the theories as well as the actual content taught in secondary schools concerning Swahili sounds and pronunciation was carried out. In the field the research was conducted in Murang'a County to find out the methodology and challenges facing teaching and learning of Swahili sounds in secondary schools. Purposive sampling was applied whereby 14 secondary schools, 2 in each of the seven sub counties in Murang'a County were selected. Six students and two teachers in each of the schools were selected to make a sample of 112 respondents. Questionnaires and a short quiz were the main devices for data collection. Data was analysed and presented through explanations, tabulations and piecharts. Statistical Package of Social Sciences Programme (S.P.S.S) was used to analyse statistical data. This research reveals that teaching of Swahili sounds and pronunciation is more emphasized in lower classes (form 1 and form 2) than in upper classes (form 3 and form 4). The study found that there is no gradual continuity of content taught in secondary schools in Kenya concerning Swahili sounds and pronunciation from one class to the other. In addition, the research explored on several challanges facing teaching of Swahili sounds and pronunciation such as; students and teachers attitudes towards Swahili sounds and pronunciation, lack of important teaching aids such as sounds recorder, mother tongue and sheng' influence among learners and teachers. The study therefore concludes that, the content on Swahili sounds and pronunciations need to be rearranged in such away there is continuity of content from one class to the other. The study will be of benefit to curriculum developers, Kiswahili teachers and lecturers. The media will also benefit from the study since they will be able to prepare students and teachers of language about good methods of learning and teaching Kiswahili sounds and their correct pronunciation.

# VIFUPISHO NA ISHARA

| | |
|---|---|
| **FZ**- | Fonolojia zalishi |
| **K**- | Konsonanti |
| **K.I.E**- | Kenya Institute of Education |
| **K.I.C.D-** | Kenya Institute of Currirulum Development |
| **KKKV-** | Konsonanti, konsonanti, konsonanti, vokali |
| **KKV**- | Konsonanti konsonanti vokali |
| **K.N.E.C**- | Kenya National Examination Council |
| **KRFZ**- | Kiunzi Rasmi cha Fonolojia Zalishi |
| **KV-** | Konsonanti vokali |
| **K.L.B-** | Kenya Literature Bereau |
| **$L_1$-** | Lugha ya kwanza |
| **$L_2$**- | Lugha ya pili |
| **S.P.E**- | Sound Pattern of English |
| **V-** | Vokali |
| **$-** | Silabi |
| ♯- | Mpaka wa silabi |
| **[ ] -** | Unukuzi fonetiki |

| | |
|---|---|
| //- | Uwasilishaji wa fonimu |

## ISTILAHI MUHIMU

**Alofoni:** Ni kipashio cha kifonolojia kinachotaja hali ambapo fonimu moja hutamkwa na kuandikwa tofauti bila kubadili maana ya neno. Alofoni ni sura au maumbo mbalimbali ya fonimu moja.

**Foni:** Ni sauti yoyote inayotamkwa na binadamu na inayoweza kutumika katika luhga fulani.

**Fonimu:** Sauti bainifu katika lugha inayotumika kuonyesha kiwango cha chini kabisa cha muundo wa kifonolojia na hutofautisha maana za maneno katika lugha mahsusi.

**Kiimbo:** Upandaji na ushukaji wa mawimbi ya sauti katika usemaji wa lugha za binadamu.

**Lugha asilia:** Lugha itumiwayo na binadamu katika mawasiliano yao.

**Lugha ya kwanza ($L_1$):** Lugha aipatayo mtu anapozaliwa na kuanza kuitumia katika mawasiliano.

**Lugha ya pili ($L_2$):** Lugha yoyote anayojifunza mtu na kuitumia kuongezea kwa lugha ya kwanza.

**Sampuli:** Idadi ndogo ya walengwa inayoteuliwa kwa utafiti kuwakilisha walengwa wote.

**Shadda:** Mkazo unaowekwa kwa silabi moja ikilinganishwa na nyingine.

**Sifa arudhi:** Ni sifa bainifu ambazo huwekwa kwenye vipashio vikubwa vya sauti Kama silabi, neno kirai na sentensi.

**Silabi:** Kipashio cha kifonolojia ambacho ni sauti au mwambatano wa sauti unaoweza kutamkika.

# YALIYOMO

UNGAMO .......... ii
TABARUKU .......... iii
SHUKRANI .......... iv
IKISIRI .......... v
ABSTRACT .......... vi
VIFUPISHO NA ISHARA .......... vii
ISTILAHI MUHIMU .......... ix
YALIYOMO .......... xi
ORODHA YA MAJEDWALI .......... xv
ORODHA YA MICHORO .......... xvii
SURA YA KWANZA .......... 1
UTANGULIZI .......... 1
1.1 Usuli wa Mada .......... 1
1.2 Suala la Utafiti .......... 4
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 4
1.4 Maswali ya Utafiti .......... 5
1.5 Sababu za kuchagua Mada .......... 5
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 7
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada .......... 9
1.7.1 Maandishi ya kijumla kuhusu dhana za Fonetiki na Fonolojia .......... 9
1.7.1.1 Dhana ya Fonetiki .......... 9
1.7.1.2 Dhana ya Fonolojia .......... 12
1.7.2. Tafiti bayana kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili .......... 17
1.8 Misingi ya Nadharia .......... 24
1.8.1 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Kielelezo cha S.P.E. .......... 24
1.8.1.1 Misingi ya Fonolojia Zalishi Kielelezo cha S.P.E. .......... 25
1.8.1.2 Mihimili ya Fonolojia Zalishi .......... 26
1.8.1.3 Sifa Pambanuzi za Chomsky na Halle .......... 27
1.8.2 Nadharia ya Utabia .......... 30
1.9 Mbinu za Utafiti .......... 32
1.9.1 Eneo la Utafiti .......... 32
1.9.2 Mbinu za Ukusanyaji Data .......... 33

1.9.2.1 Hojaji ..... 33
1.9.2.2 Mazoezi Andishi ..... 38
1.9.3 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti ..... 38
1.9.4 Usampulishaji ..... 38
1.9.5 Uchanganuzi wa Data ..... 40
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ..... 40
1.9.7 Uzingatifu wa Maadili ..... 41
1.10 Hitimisho ..... 41
SURA YA PILI ..... 42
UFUNZAJI WA MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI ..... 42
2.0 Utangulizi ..... 42
2.1.0 Silabasi ya Kiswahili na Ufunzaji wa Matamshi ya Kiswahili katika Shule za Upili nchini Kenya ..... 43
2.1.1 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Kwanza ..... 44
2.1.2 Mahitaji ya Silabasi kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Pili ..... 47
2.1.3 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha tatu ..... 48
2.1.4 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Nne ..... 49
2.2 Mada za Matamshi ya Kiswahili katika Vitabu vya Kiada katika Shule za Upili Nchini Kenya ..... 51
2.2.1 *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018) ..... 51
2.2.2 *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018) ..... 53
2.2.3 *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) ..... 54
2.2.4 *Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015) ..... 55
2.3. Hitimisho ..... 58
SURA YA TATU ..... 60
MBINU ZA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA ..... 60
3.0 Utangulizi ..... 60
3.1 Hojaji kwa walimu ..... 60
3.2 Hojaji kwa wanafunzi ..... 61
3.3 Hitimisho ..... 64
SURA YA NNE ..... 65
CHANGAMOTO ZA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI ..... 65

4.0 Utangulizi ........ 65
4.1.0 Hojaji kwa walimu ........ 65
4.1.1 Kiwango cha Elimu ........ 65
4.1.2 Tajriba ya Ufunzaji Kimiaka ........ 66
4.1.3 Mwelekeo kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili ........ 67
4.1.4 Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili ........ 69
4.1.5 Changamoto nyingine zinazoathiri Ufunzaji wa Matamshi ya Kiswahili ........ 70
4.1.6 Hatua Faafu za Kuboresha ufunzaji matamshi ya Kiswahili ........ 74
4.2.0 Hojaji kwa Wanafunzi ........ 74
4.2.1 Ni lini mara ya kwanza ulikabiliana na sauti za Kiswahili ........ 74
4.2.2 Mtazamo wa Somo la Sauti za Kiswahili ........ 75
4.2.3 Ugumu wa Somo la Sauti ........ 76
4.2.4 Ni Mara ngapi unafanya Mazoezi yanayohusu Sauti ya Kiswahili ........ 77
4.2.5 Changamoto nyingine katika Kusoma Sauti za Kiswahili ........ 78
4.2.6 Jinsi ya kuboresha ujifunzaji wa sauti za Kiswahili ........ 79
4.3.0 Zoezi kwa Wanafunzi ........ 79
4.3.1 Matokeo ya Zoezi kwa kila Kidato ........ 79
4.3.2 Matokeo ya kila Swali katika Zoezi kwa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza ........ 80
4.3.3 Matokeo ya kila Swali katika Zoezi kwa Wanafunzi wa Kidato cha Nne ........ 84
4.4 Hitimisho ........ 90
SURA YA TANO ........ 91
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO ........ 91
5.0 Utangulizi ........ 91
5.1 Muhtasari ........ 91
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 94
5.3 Mapendekezo ........ 102
5.4 Matatizo ........ 105
5.5 Hitimisho ........ 106
MAREJELEO ........ 108
KIAMBATISHO 1: HOJAJI KWA WANAFUNZI ........ 111
KIAMBATISHO 2: ZOEZI KWA WANAFUNZI ........ 114
KIAMBATISHO 3: HOJAJI KWA WALIMU ........ 115

KIAMBATISHO 4: RATIBA YA KAZI KUTOKA MEI 2017 HADI MACHI, 2021 ................................ 117
KIAMBATISHO 5: MAKADIRIO YA BAJETI YA UTAFITI.................................................................. 118
KIAMBATISHO 6: IDHINI YA KUKUSANYA DATA YA NYANJANI .................................................. 119
KIAMBATISHO 7: SAMPULI YA MAZOEZI YA WANAFUNZI YALIYOSAHIHISHWA ........................ 121
KIAMBATISHO 8; MAJALADA YA VITABU VYA KIADA VILIVYOIDHINISHWA KUFUNZIA SOMO LA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI KENYA .................................................................................... 123

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 1:** Ripoti ya matokeo ya mtihani wa Kiswahili wa kitaifa KNEC, KCSE, 2014

**Jedwali 2:** Mada za matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza

**Jedwali 3:** Mada za matamshi ya Kiswahili katika kidato cha pili

**Jedwali 4:** Mada za matamshi ya Kiswahili katika kidato cha tatu

**Jedwali 5:** Mada za matamshi ya Kiswahili katika kidato cha nne

**Jedwali 6:** Kiwango cha elimu

**Jedwali 7:** Tajriba ya ufunzaji kimiaka

**Jedwali 8:** Mwelekeo kuhusu ufunzaji matamshi ya Kiswahili

**Jedwali 9:** Mwelekeo wa wanafunzi kuhusu ufunzaji matamshi ya Kiswahili

**Jedwali 10:** Changamoto zinazoathiri ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili

**Jedwali 11:** Ni lini mara ya kwanza ulikabiliana na sauti za Kiswahili?

**Jedwali 12:** Mtazamo wa wahojiwa kuhusu somo la sauti za Kiswahili

**Jedwali 13:** Ugumu wa somo la sauti

**Jedwali 14:** Mbinu za kujifunza sauti za Kiswahili

**Jedwali 15:** Ni mara ngapi unafanya mazoezi yanayohusu sauti za Kiswahili

**Jedwali 16:** Matokeo ya jumla ya zoezi kwa wanafunzi kwa kila kidato

**Jedwali 17:** Swali la kwanza (Tofauti ya irabu na konsonanti)

**Jedwali 18:** Swali la pili (Sifa za fonimu za irabu)

**Jedwali 19:** Swali la tatu (Mkazo/Shadda)

**Jedwali 20:** Swali la nne (sifa za fonimu za konsonanti)

**Jedwali 21:** Swali la tano (kutenga silabi)

**Jedwali 22:** Swali la sita (Sauti tata /f/ na /v/)

**Jedwali 23:** Swali la saba (Miundo ya silabi)

**Jedwali 24:** Swali la nane (Kiimbo)

**Jedwali 25:** Swali la tisa (Sifa bainifu za konsonanti)

**Jedwali 26:** Swali la kwanza (Tofauti ya irabu na konsonanti)

**Jedwali 27:** Swali la pili (Sifa za fonimu za irabu)

**Jedwali 28:** Swali la tatu (Mkazo/Shadda)

**Jedwali 29**: Swali la nne (sifa za fonimu za konsonanti)

**Jedwali 30:** Swali la tano (kutenga silabi)

**Jedwali 31:** Swali la sita (Sauti tata /f/ na /v/)

**Jedwali 32:** Swali la saba (Miundo ya silabi)

**Jedwali 33:** Swali la nane (Kiimbo)

**Jedwali 34:** Swali la tisa (Sifa bainifu za konsonanti)

## ORODHA YA MICHORO

**Mchoro 1:** Mgao wa wahojiwa kutegemea kiwango cha kidato

**Mchoro 2:** Mgao wa wahojiwa kutegemea kiwango cha maeneo cha Kaunti ndogo

**Mchoro 3:** Mgao wa wahojiwa kutegemea kategoria za shule – kutwa au bweni

**Mchoro 4:** Mgao wa wahojiwa kutegemea kategoria za shule – wasichana, wavulana au mseto.

**Mchoro 5:** Mgao wa wahojiwa kulingana na viwango vya shule.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Lugha ya Kiswahili nchini Kenya imepewa hadhi ya juu ikilinganishwa na lugha nyingine. Kwa sasa Kiswahili ni lugha ya taifa, lugha rasmi, na tayari lugha hii ina wajibu mkubwa wa kimataifa. Aidha, Kiswahili kimekua kwa kiasi kikubwa kikitumika katika sayansi na teknolojia. Kwa kweli, lugha hii imepata umaarufu nchini Kenya. Hata hivyo, lugha hii ambayo wengi hujifunza kama lugha ya pili ($L_2$) imekumbwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo huoanishwa na ufunzaji na ujifunzaji wake. Nchini Kenya lugha ya Kiswahili hufunzwa na kutahiniwa kama lugha ya lazima katika shule za msingi na shule za upili kote. Lugha hii ni chombo muhimu cha mawasiliano, biashara, dini, siasa miongoni mwa mengine nchini Kenya.

Wanaisimu wengi kama vile Trudgil (1974) wanakubaliana kwamba lugha ya binadamu ni mfumo wa sauti nasibu unaotumiwa na jamii ya watu kwa lengo la kuwasiliana. Kwa kuzingatia fasili hii ni dhahiri kuwa mhimili mkuu wa lugha asilia ni sauti. Sauti za lugha hufafanuliwa katika matawi ya fonetiki na fonolojia ambayo huhusiana (Massamba na wenzake, 2004). Kwa kawaida ujifunzaji lugha hutokea kwa viwango mbalimbali ambavyo ni sauti, neno, sentensi, maana na matumizi ya lugha yenyewe yaani viwango vya fonetiki na fonolojia (sauti), mofolojia (neno),

sintaksia (sentensi), semantiki (maana) na pragmatiki (matumizi ya lugha). Matawi ya fonetiki na fonolojia ndiyo msingi wa matawi hayo mengine yote ya isimu.

Kiisimu, fonetiki ni tawi linaloshughulika na uchunguzi, uchambuzi wa taratibu zote zinazohusiana na utoaji, utamkaji, usafirishaji, usikiaji na utambuzi wa sauti za lugha ya binadamu kwa jumla (Massamba na wenzake, 2004). Taaluma hii huchunguza sauti zote zinazoweza kutumika katika lugha yoyote ile bila kujali zinatumika katika lugha gani. Kindija (2012) anasema kwamba fonetiki ni lazima kwa mtu anayetarajia kujifunza isimu na ni vigumu mwanadamu kufafanua sarufi ya lugha fulani iwapo hawezi kusikia na kunukuu sauti na maneno yake. Kindija (2012) anadai kuwa walimu wa lugha lazima wawe na ujuzi wa fonetiki ili kusaidia wanafunzi wao.

Fonolojia nayo imefafanuliwa kwa njia tofauti na wanaisimu mbalimbali. TUKI (1990) wanasema kuwa fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumiwa katika lugha fulani. Mgullu (1999) anajumlisha maoni ya wataalamu waliotangulia na kudai kuwa kuna matawi mawili ya fonolojia; fonolojia vipande na fonolojia arudhi. Mgullu (1999) anaeleza kuwa fonetiki na fonolojia ni matawi jirani na hutegemeana kila wakati kwani yote yanachunguza sauti. Anasema kuwa uchambuzi wa fonetiki husaidia uchambuzi wa fonolojia na vile vile uchambuzi wa fonolojia husaidia uchambuzi wa fonetiki. Katika ujifunzaji wa fonolojia ya lugha mahususi mwanafunzi anajifunza mfumo wa sauti za lugha hiyo

ili aweze kufahamu namna sauti hizo zinavyoungana hata kuunda vipashio vikubwa kuliko sauti kama silabi, maneno na sentensi.

Ufunzaji na ujifunzaji wa mada zinazohusu sauti na matamshi bora ya Kiswahili katika shule za upili haujatiliwa maanani licha ya kupendekezwa na silabasi mpya ya Kiswahili ya sekondari ya K.I.C.D. ya 2006 pamoja na mwongozo wa baraza la mitihani (KNEC). Tarone (1987) anadai kwamba taaluma ya fonolojia inaelekea kufifia ikilinganishwa na matawi mengine ya isimu kama vile mofolojia, sintaksia na semantiki katika ujifunzaji na ufunzaji wa lugha yoyote ya pili. Hii ni kwa sababu watafiti, walimu na wanafunzi kwa ujumla hawachukulii masuala ya matamshi bora kwa uzito.

Katika kaunti ya Murang'a, somo la Kiswahili hasa karatasi ya pili 102/2 limekuwa likiripoti matokeo mabaya mwaka baada ya mwaka katika mitihani ya kitaifa. Kwa mfano, kulingana na takwimu za Wizara ya Elimu, Kaunti ya Murang'a, K.C.S.E. 2014 ni asilimia 17.33 pekee ya shule za upili zilizoweza kufikisha alama ya wastani ya 6.0 katika somo la Kiswahili. Katika kaunti ndogo ya Gatanga K.C.S.E. 2015 ni asilimia 6 pekee ya shule zote katika kaunti ndogo hiyo waliofikisha alama ya 6.0 katika somo la Kiswahili. Hivyo basi kuna uwezekano wa dosari kubwa katika ujijfunzaji na ufunzaji wa sarufi ya Kiswahili ambayo misingi yake ni sauti na matamshi bora.

Tafiti za awali zinazohusu ufunzaji wa lugha ya Kiswahili kama vile Mbaabu (1995), King'ei na Musau (2002) miongoni mwa nyingine zimeonyesha kujitokeza kwa

makosa katika viwango vya kifonolojia, mofolojia na sintaksia wanafunzi wanapojifunza Kiswahili. Makosa bado hujitokeza licha ya baadhi ya mapendekezo kutekelezwa. Otiende (2013) alipendekeza walimu wa lugha ya Kiswahili kutilia maanani mafundisho kamili ya fonolojia ya Kiswahili hasa madarasa ya chini ili kuweka msingi imara wa matumizi na ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti huu unalenga kutathmini ufunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili katika kaunti ya Murang'a Kenya.

### 1.2 Suala la Utafiti

Kulingana na Chieni (2001) ufunzaji matamshi na maandishi ya Kiswahili hausisitizwi vya kutosha katika shule za upili nchini Kenya. Alilalamikia Kiswahili kutopewa hadhi sawa na Kingereza katika mfumo wa elimu. Mbaabu (1995) anaeleza kuwa baadhi ya makosa ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi huingiliana na kuathiriana. Kingei na Musau (2002) walitafiti kuhusu utata wa Kiswahili na kubaini kuwa wazungumzaji wasiotumia matamshi sahihi ya Kiswahili hawaeleweki vizuri kimaana kila mara. Isitoshe, kipengele cha matamshi au mazungumzo hakitahiniwi katika mitihani ya kitaifa. Ni kwa misingi hii basi tulilenga kutathmini ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya kwa kuongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi kielelezo cha S.P.E. na nadharia ya Utabia.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Kwa ujumla utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

i) Kutathmini yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili.

ii) Kubainisha mbinu za ufunzaji matamshi katika shule za upili.

iii) Kuchunguza changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili.

Kwa mujibu wa malengo haya, utafiti ulinuia kujibu maswali kadha kuwezesha malengo yote kufikiwa.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i) Ni yapi yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi ya Kiswahili?

ii) Ni mbinu zipi zinazotumika kufunza matamshi ya Kiswahili katika shule za upili?

iii) Ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili una changamoto zipi?

**1.5 Sababu za kuchagua Mada**

Tafiti zilizofanywa kuhusiana na lugha na isimu ya Kiswahili zinalenga maneno, makosa ya kisarufi katika Kiswahili, sintaksia na fonolojia ya Kiswahili kwa ujumla na ujifunzaji wa aina za maneno kama vile nomino, vibainishi, vivumishi na vitenzi. Kwa ufahamu wetu, nafasi ya utafiti wa masuala halisi yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi ya Kiswahili, mbinu na changamoto za ufunzaji matamshi haijazingatiwa na tafiti za awali. Utafiti huu basi umeziba pengo hili kwa kushughulikia ufunzaji halisi wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili.

Wanaisimu kama Mbaabu (1995), King'ei na Musau (2002) wamejikita zaidi katika kuonyesha aina za makosa ya matamshi na athari zake katika ujifunzaji lugha pasi kujikita kwa undani katika ufunzaji halisi wa matamshi.

Aidha, kama matawi msingi yanayojenga matawi hayo mengine ya lugha hatukuwa na budi kuyatafitia ili kuongeza maarifa katika taaluma hii inayohusu sauti na ambayo haijafanyiwa utafiti wa kutosha (Chieni, 2001). Vile vile, silabasi ya Kiswahili katika shule za upili hupendekeza ufunzaji wa mada ya kusikiliza na kuzungumza inayohusisha vipengele vya sauti na matamshi ya Kiswahili na hivyo haja ya kutafiti mbinu na changamoto zilizomo. Kwa vile wanafunzi wengi nchini Kenya hujifunza Kiswahili kama $L_2$, utafiti huu ulijikita katika ufunzaji matamshi ili kusaidia kutambua makosa yanayoletwa na utamkaji mbaya wa vitamkwa vya Kiswahili kutokana na $L_1$ ya wanafunzi na hatimaye kupendekeza mbinu za kuboresha.

Kulingana na takwimu za KNEC (2014), matokeo ya mtihani wa Kiswahili yamekuwa yakiyumbayumba mwaka baada ya mwingine tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya (2006). Wanafunzi wengi walirekodi alama ya chini ya wastani yaani 2011 (43.45), 2012 (29.06), 2013 (29.92) na 2014 (32.27) katika somo la Kiswahili karatasi ya pili 102/2 mtihani wa kitaifa. Karatasi ya pili inahusika na sarufi ya Kiswahili ambayo ina nguzo kuu katika matamshi na fonolojia ya Kiswahili kwa jumla na hivyo kushawishika kutathmini ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

Tuna matumaini kuwa utafiti huu utawafaa walimu wa shule za upili katika kaunti ya Murang'a na kwingineko kutambua matatizo na mbinu za kufunza matamshi na

fonolojia ya Kiswahili shuleni. Wakuza mitalaa, waandishi na wapenzi wa lugha ya Kiswahili watanufaika kutokana na utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika kukuza taaluma ya sauti na matamshi ya Kiswahili.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kaunti ya Murang’a ili kubaini yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kwa mujibu wa silabasi, changamoto pamoja na mbinu zinazotumiwa kufunza na kujifunza matamshi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu kaunti ya Murang’a imeripotiwa kuzoa matokeo mabaya ya mitihani ya kitaifa K.C.S.E. hasa katika somo la Kiswahili ambapo asilimia 83% ya shule za upili katika kaunti yote hazikufikisha alama ya wastani 6.0 katika somo hilo (Ripoti ya matokeo ya mitihani ya kitaifa kaunti ya Murang’a 2014). Ripoti ya matokeo ya mtihani wa Kiswahili K.C.S.E 2014, yanadhihirisha kuwa karatasi ya pili 102/2 ndiyo iliyofanywa vibaya zaidi ikilinganishwa na 102/1 na karatasi ya 102/3 ambazo zilikuwa juu ya wastani kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 1.

**Jedwali 1: Ripoti ya Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kitaifa wa KNEC, KCSE, 2014**

| Mwaka | karatasi | watahiniwa | Upeo | Alama ya wastani | Alama tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | 102/1 | 482122 | 40 | 20.17 | 5.26 |
| | 102/2 | | 80 | 32.27 | 12.60 |
| | 102/3 | | 80 | 42.93 | 15.81 |

(Kutoka: Ripoti ya mitihani ya kitaifa ya KNEC, KCSE, 2014)

Ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili ni mojawapo ya masomo msingi ambayo hufunzwa katika vidato vyote katika vijimada vya kusikiliza na kuzungumza, matamshi bora, kusoma na kuandika. Mengi yanayohusu matamshi hasa utamkaji wa fonimu, miundo ya silabi za Kiswahili, shadda na kiimbo hufunzwa katika kidato cha kwanza muhula wa kwanza. Utafiti huu ulihusisha wanafunzi wa kidato cha kwanza na wale wa kidato cha nne. Hili lilisaidia kuchunguza umilisi wa sauti na matamshi ya Kiswahili katika kiwango cha chini (kidato cha kwanza) ikilinganishwa na kile cha juu (kidato cha nne). Aidha, walimu wenye tajriba ya ufunzaji wa Kiswahili walihusishwa katika utafiti ili kubainisha mbinu wanazotumia kufunzia pamoja na changamoto wanazokumbana nazo katika ufunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili.

Utafiti wetu ulitumia vitabu vinne; yaani kitabu kimoja kwa kila kidato ambavyo ni *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili*

*Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) na *Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015) ili kuchunguza masuala yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili na kutathimini kama masuala yanayofunzwa yanaoana na mapendekezo ya silabasi ya Kiswahili (K.I.E, 2002). Lengo letu la kuchagua vitabu hivi maalum vya kiada ni kwa sababu vitabu hivi ndivyo vilivyoidhinishwa na K.I.C.D. na kugharamiwa na serikali ya Kenya kwa kila mwanafunzi kufunzia Kiswahili na hasa mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Maelezo kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada yamewasilishwa kwa vipengele viwili, yaani; maandishi ya kijumla kuhusu taaluma ya fonetiki na fonolojia na tafiti bayana kuhusu ujifunzaji na ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

### 1.7.1 Maandishi ya kijumla kuhusu dhana za Fonetiki na Fonolojia

Katika sura ya kwanza, tulidokeza kuwa suala la matamshi ya lugha, linahusika na matawi ya fonetiki na fonolojia. Matawi ya fonetiki na fonolojia ya lugha yoyote ile hujenga msingi wa matawi mengine ya lugha husika. Kutokana na wazo hili, tumelenga kufafanua kwa utondoti dhana za fonetiki na fonolojia ili kueleweka kwa wepesi.

#### 1.7.1.1 Dhana ya Fonetiki

Dhana ya fonetiki na dhana ya fonolojia ya Kiswahili zimeshughulikiwa na wanaisimu pamoja na watafiti tofauti tofauti. Kwa mfano, Massamba na wenzake

(2004) wameshughulikia suala la fonetiki kwa upana. Wanasema kuwa fonetiki ni tawi la isimu linaloshughulika na uchunguzi na uchambuzi wa taratibu zote zinazohusiana na utoaji, utamkaji, usafirishaji, usikiaji na utambuzi wa sauti za lugha ya binadamu kwa jumla. Taaluma hii huchunguza sauti zote zinazoweza kutumika katika lugha yoyote ile bila kujali zinatumika katika lugha gani au kwa njia gani. Kwa mwanaisimu, fonetiki ni ya lazima. Ni vigumu mwanaisimu kufafanua sarufi ya lugha kama lugha yenyewe hawezi kuisikia na kunukuu sauti na maneno yake. Mtu yeyote baada ya kufahamu na kuielewa fonetiki anaweza kujifunza lugha yoyote bila shida ya kutamka (Kindija, 2012:5).

Aidha, Kindija (2012) anadai kuwa walimu wa lugha lazima wawe na ujuzi wa fonetiki ili kusaidia wanafunzi wao. Anaendelea kusema kuwa makosa ya kimatamshi hayafanywi kimaksudi bali wanafunzi huwa hawasikii au hawapambanui vyema tofauti kati ya matamshi yake ghafi na matamshi safi ya mwalimu. Kindija anadai kuwa fonetiki ni taaluma nyeti na pana. Fonetiki si taaluma ya kinadharia. Hii ni taaluma ya utendaji na ni lazima mafunzo yake yaandamane na mazoezi ya utamkaji na usikilizaji (Kindija, 2012:31).

Kindija (2012) anasema kuwa taaluma ya fonetiki ina matawi mengi kama vile fonetiki masikizi, fonetiki matamshi, fonetiki tiba-matamshi, fonetiki akustika na fonetiki majaribio. Kindija (2012:19) anaeleza kuwa fonetiki masikizi ni tawi dogo la fonetiki linalohusu uchunguzi na uchanganuzi wa namna sauti za lugha zinavyokamatwa na sikio zikasafirishwa kwenda kwenye ubongo kupitia neva

zinazohusika na usikiaji. Aanaendelea kufafanua kuwa mawasiliano kwa njia ya upitishaji wa mawazo au hisia hutoka katika akili ya msemaji hadi akili ya msikilizaji. Hili ni tawi la fonetiki linaloshughulikia jinsi mawimbi ya sauti yanavyoingia katika sikio la msikilizaji na kusafirishwa na ubongo wake hata kuopata maana.

Crystal (1989) anasema kuwa fonetiki matamshi hujulikana kama fonetiki fiziolojia. Anaendelea kusema kuwa katika fonetiki matamshi, sauti zinaainishwa kufuatana na vigezo vikuu viwili; mahali zinatamkiwa na jinsi sauti hizo zinavyotamkwa. Hivyo basi kinachoangaliwa hapa ni jinsi ya utamkaji wa sauti, mahali pa matamshi na hali ya mkondo hewa (kama ni ghuna au sighuna).

Fonetiki akustika, kulingana na Kindija (2012), ni tawi la kifonetiki linalojishughulisha na uchunguzi wa namna sauti za lugha zinavyosafiri kutoka kwa msemaji hadi kwenye sikio la msikilizaji. Aghalabu uchunguzi na uchanganuzi huu huhitaji matumizi ya vifaa vya kielektroniki.

Massamba na wenzake (2004) walidai kuwa kuna tawi la nne la kifonetiki liitwalo fonetiki tiba matamshi. Mgullu (1999) analiita tawi hili fonetiki majaribio. Tawi hili linashughulikia matatizo yanayoambatana na usemaji na jinsi ya kuyatatua. Kindija (2012) anakubaliana na sababu za kuchagua mada ya utafiti huu kwamba uwanja wa fonetiki haujafanyiwa utafiti wa kutosha hasa ufunzaji wake shuleni.

Hyman (1975) anafasili fonetiki kama taaluma ambayo hususan huchunguza sauti ambazo hutumika na wanadamu wakati wanapowasiliana kwa kutumia lugha.

Anasema kuwa ufunzaji wa fonetiki huwa haujihusishi na lugha yoyote maalum na kutokana na hali hiyo kipashio kinachotumiwa katika uchambuzi wa fonetiki ni foni. Hyman (1975) anaeleza foni kama kipashio muhimu cha fonetiki. Anasema kuwa foni ni sauti yoyote inayotamkwa na binadamu na inayoweza kutumika katika lugha fulani. Foni ni nyingi sana na hazina maana yoyote. Wanaisimu hawa walichangia utafiti huu kwa kuweka msingi dhahiri wa dhana ya fonetiki.

#### 1.7.1.2 Dhana ya Fonolojia

Kama ilivyo fonetiki, wanaisimu tofauti tofauti wamefasili maana ya fonolojia. Fudge (1973) anadai kuwa fonolojia ni kiwango mojawapo cha lugha fulani kilicho na vipashio vingine vidogo zaidi kuliko vipashio vingine vyote vya lugha. Vipashio hivyo ni fonimu, alofoni na silabi. Hartman (1972) anasema kwamba fonolojia ni mtalaa wa sauti zinazotumiwa katika lugha fulani na uamilifu wa ndani ya mfumo wa lugha inayohusika.

Massamba na wenzake (2004) wanasema kuwa fonolojia ni tawi la isimu ambalo hushughulika na uchunguzi, uchambuzi na uainishaji wa sauti pambanuzi ambazo hutumika katika mifumo mbalimbali ya sauti za lugha ya binadamu. Ina maana kuwa fonolojia hushughulikia hasa zile sauti ambazo hutumika kutofautisha maana za maneno katika lugha mahususi. Fonolojia kama taaluma ya isimu hujishughulisha na vipengele mbalimbali kama vile matamshi, kiimbo, mkazo, lafudhi, wakaa, toni, mfuatano wa sauti kuunda silabi, mfuatano wa silabi kuunda mofimu na mfuatano

wa mofimu kuunda maneno. Massamba na wenzake (2004) wanaendelea kusema kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya fonolojia na uundaji wa maneno.

Massamba na wenzake walishughulikia dhana ya kitamkwa na kusema fonimu ni kitamkwa kilicho bainifu katika lugha fulani maalum. Kuna aina tatu kuu za vitamkwa; irabu, konsonanti na viyeyusho (Massamba na wenzake 2004). Massamba (2010) anasema kuwa fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulika na mfumo wa sauti (asilia) za lugha. TUKI (1990) wanasema kuwa fonolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti katika lugha fulani.

Mgullu (1999) anajumlisha maoni ya wataalamu waliomtangulia na kusema kuwa fonolojia inaweza kuwa na sura mbili kuu. Fonolojia vipande na fonolojia arudhi. Fonolojia vipande hushughulikia uchunguzi wa vipande sauti yaani kubainisha vipande sauti bainifu katika lugha fulani; fonimu na alofoni zake, kutumia sifa bainifu, kuzifafanua fonimu na alofoni hizo. Fonolojia arudhi hushughulika na masuala ya sauti yanayoathiri vipashio vikubwa zaidi kuliko fonimu kama vile mkazo, toni, kiimbo na silabi za lugha fulani. Utafiti wetu umejikita katika vipengele hivi viwili vya kifonolojia (taz.1.6-upeo na mipaka)

Mgullu (1999) anasema kuwa matawi mengine ya taaluma ya fonolojia ni kama vile fonolojia asilia. Huu ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha ambao husisitiza umuhimu wa kuzingatia taratibu asilia za usemaji wa lugha. Lengo ni kuchunguza sheria, kanuni, michakato na taratibu mbalimbali zinazojitokeza katika lugha zote za ulimwengu na ambazo hazina budi kufuatwa katika uchanganuzi wa fonolojia ya lugha. Fonolojia asilia zalishi nao ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha asilia ambao unasisitiza kuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja baina ya uwakilishwaji wa maumbo mbalimbali ya ndani (pamoja na sheria zinazoendana nayo) na yale ya nje.

Fonolojia leksika kwa mujibu wa Mgullu (1999) ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha ambao kwao baadhi ya sheria za kifonolojia huhamishiwa katika sehemu ya leksika na kuwa sehemu ya mofolojia. Mgullu (1999) anaeleza kuwa fonolojia mizani ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha ambao umekitwa katika mfumo wa sauti za lugha kama kitu ambacho kimejengeka kimsonge kwa kufuata msingi wa silabi lakini chenye uhusiano wa viwango tofauti kati ya vipengele vyake.

Fonolojia umbo upeo *(optimal phonology)* ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha ambao umekitwa kwenye madai kwamba miundo mbalimbali ya lugha hutokana na mashartizuizi ya kimajumui yaliyomo katika lugha za binadamu. Madai haya nayo yamekitwa kwenye mtazamo kwamba tofauti zinazojitokeza katika lugha za binadamu hutokana na tofauti za uthamini wa mashartizuizi hayo.

Fonolojia vipambasauti ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa sauti za lugha asilia wa vipengele ambavyo huvuka mipaka ya vipandesauti; yaani vipashio kama toni, mpandoshuko, lafudhi, kidatu, mkazo na tempo ( Mgullu, 1999). Fonolojia vipandesauti huruni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha asilia ambao umekitwa katika msingi kwamba kila

kipandesauti (kitamkwa, mkazo, toni, na kadhalika) hujitegemea na huwa katika rusu yake yenyewe (si sehemu ya kingine).

Fonolojia zalishi kwa mujibu wa Mgullu (1999), ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha asilia ambao nia na lengo lake ni kujaribu kubainisha sheria na kanuni za kimajumui zinazohusisha umbo ndani na umbo nje la mfumo wa sauti.

Fonolojia zalishi asilia ni mtazamo wa kinadharia katika uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha asilia ambao unaamini kwamba wasemaji wa lugha yoyote iwayo, katika usemaji wao huwa wanajikita katika majumuisho ambayo yanadhihirika katika kinachosemwa na kuleta uangavu wa kilichokusudiwa.

Mgullu (1999) anagawa fonimu za Kiswahili kwa aina tatu kuu. Fonimu za irabu, fonimu za nusu irabu na fonimu za konsonanti. Anadai kuwa Kiswahili kina fonimu thelathini na moja kwa jumla. Tano za irabu, ishirini na nne za konsonanti na fonimu mbili za nusu irabu. Fonimu za irabu za Kiswahili ni; / a/,/e/,/i/ /o/ na ,/u/. Fonimu za nusu irabu ni /w/ na/ y/ nazo fonimu za konsonanti ni; /b/, /ch,//d/,/dh/,/f/,/ g /,/gh/,/h/,/ k/,/ l/,/m/,/n/,/ng’ /,/ny/,/p/, /r/, /s/, /sh/, /t/, /th/, /f/, /v/ ,/z/, na /kh/. Kila fonimu ya Kiswahili ina sifa zake bainifu.

Lipo tatizo ambalo halijapata ufumbuzi linalohusiana na fonimu za konsonanti za Kiswahili. Tatizo la mwambatano wa fonimu nyingine. Konsonanti fulani huungana kuunda fonimu moja. Kwa mfano neno ndama laweza kufasiliwa kwa namna mbili;

i) Lina fonimu nne yaani /n/+/d/+/a/+/m/+/a/

ii) Lina fonimu tatu /nd/+/a/+/m/+/a/ Mgullu (1999:69)

Mgullu (1999) aidha alishughulikia suala la silabi kama fonolojia arudhi. Alisema kila lugha ina silabi zake. Aligawa silabi kwa aina mbili; yaani silabi wazi na silabi funge. Anakubaliana na wanafonolojia wengine kuwa silabi zina sehemu tatu kuu; kilele, mwanzo na koda. Anasema silabi ni muhimu kwani husaidia kubeba sifa mbalimbali za kiarudhi katika lugha fulani kama vile mkazo na toni. Vile vile Mgullu (1999) alishughulikia miundo ya silabi za Kiswahili. Mgullu anasema kuwa mkazo katika maneno ya Kiswahili ni mkazo fungwa kwani huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho.

Massamba na wenzake (2004) walishughulikia miundo ya silabi za Kiswahili kama kipashio cha kifonolojia kinachohusu matamshi. Wanasema kuwa maneno hutamkwa kwa utaratibu wa silabi. Kwa mfano-$u$$a$. Polome (1967) ametalii sana masuala ya fonolojia ya Kiswahili sanifu. Maelezo yake yalikuwa na manufaa sana kwetu. Aidha alishughulikia uainishaji fonimu.

Lass (1984) ameeleza mifumo ya kifonolojia, ala za matamshi na sifa bainifu za fonimu. Iribe mwangi (2010) ametoa sifa bainifu za fonimu na mifanyiko ya

kifonolojia katika Kiswahili sanifu. Wataalamu hawa walichangia ufahamu wa misingi ya fonolojia ya Kiswahili ambayo ni muhimu sana katika utafiti wetu. Hata hivyo, wanaisimu hawa wote walishughulikia fonolojia ya Kiswahili kwa ujumla bila kujikita katika ufunzaji wake shuleni, mbinu zinazotumiwa na changamoto wanazokumbana nazo wanaojifunza taaluma hii. Utafiti wetu basi ulinuia kuziba pengo hilo.

### 1.7.2. Tafiti bayana kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili

Tafiti za awali, licha ya kuchangia ufahamu wa misingi ya fonolojia ya Kiswahili ambayo ni muhimu katika utafiti wetu, zilishughulikia fonolojia ya Kiswahili kwa ujumla bila kujikita katika ufunzaji wake shuleni, mbinu zinazotumiwa na changamoto wanazokumbana nazo wanaojifunza taaluma hii. Utafiti huu basi ulinuia kuziba pengo hili. Baadhi ya tafiti hizo ni kama zifuatazo:

Musau (1993) aliendeleza utafiti wake katika fonolojia ya Kiswahili na kushughulikia makundi ya lugha yafuatayo; Kinandi, Kikamba, Kikuyu, Kibukusu, Kisomali, Kimaasai na Kiluo. Katika utafiti wake aliainisha jinsi wazungumzaji wa lugha hizi wanavyoathiriwa na lugha zao za kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Sampuli yake ilikuwa ni wanafunzi katika vyuo vya walimu wa shule za msingi ambavyo ni Thogoto, Highridge na Machakos.

Hata hivyo, utafiti wa Musau (1993) ni tofauti na wetu kwa sababu kadhaa. Kwanza Musau alishughulikia sampuli pana ya lugha saba. Aidha, Musau alihusisha wanafunzi wa vyuo vya walimu lakini utafiti wetu ulihusisha wanafunzi

wa shule za upili. Vile vile, utafiti wa Musau haukulenga hali ya ufunzaji wa fonetiki na fonolojia ya Kiswahili yaani mbinu na changamoto zinazokumba ufunzaji wa mada hizi. Utafiti wake hivyo basi uliacha pengo ambalo utafiti wetu ulishughulikia.

Mbaabu (1995) amegawa makosa yanayofanywa na watu wengi katika Kiswahili kwa makundi matatu; yaani makosa ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi. Anaendelea kusema kuwa makundi haya huingiliana hivi kwamba kosa la kimatamshi laweza kuwa la kisarufi na vile vile kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Baadhi ya makosa ya kimaandishi husababishwa na makosa ya kimatamshi. Mbaabu (1995), anasema kuwa makosa mengi ya kimatamshi husababishwa na maingiliano ya L1 pamoja na unyonge wa kutojitahidi kutamka maneno jinsi yanavyojitokeza katika maandishi. Mbaabu ametumia ulinganishi wa jozi finyu kuonyesha wazi matatizo ya kimatamshi yanavyopotosha maana kwa kutumia maneno halisi. Ametumia sauti tatanishi kama vile /p/ na /b/ /ch/ na /j/ /f/ na /v/ /w/na /y/ miongoni mwa nyingine.

Mbaabu (1995), mbali na kuonyesha utata wa matamshi ya Kiswahili waziwazi na aina za makosa ya kimatamshi, hakushughulikia suala la ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi shuleni.

Chieni (2001) anasema kuwa ufunzaji wa matamshi na maandishi ya Kiswahili usisitizwe. Analalamika kuwa Kiswahili hakijapewa hadhi sawa na Kiingereza katika mfumo wa elimu. Analinganisha hadhi ya Kiswahili na Kingereza na

kugundua kuwa Kiswahili kilipewa nafasi finyu katika shule za upili na vyuo vikuu. Utafiti huu ulishughulikia changamoto za ufunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa ujumla tu bila kuzingatia mbinu za ufunzaji tofauti na ilivyo katika utafiti wetu.

Utafiti unaokaribiana na wetu ni ule wa Musau na Chacha (2001). Wao wamezungumzia mbinu za kufunza matamshi ya Kiswahili. Wanakubaliana na watafiti wengine kwamba matatizo ya kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili nchini Kenya yana asili tofauti tofauti lakini asili kuu ni athari za lugha ya kwanza. Wanasema kuwa mwalimu anayefundisha matamshi ya Kiswahili sanifu anapaswa kuwa na ufahamu wa fonolojia za $L_1$ za wanafunzi wake. Hili litasaidia mwalimu kulinganisha sauti za lugha mama za wanafunzi pamoja na lugha ya Kiswahili na hivyo kuweza kubashiri matatizo ya matamshi yanayoweza kuwakumba wanafunzi wake. Ili kufahamu mfumo wa sauti za lugha ya mwanafunzi, mwalimu atahitaji ufahamu wa masuala ya vitamkwa vya lugha, vitamkwa vinavyotegemea mazingira, mpangilio wa vitamkwa vya lugha, viungo vinavyohusika na matamshi pamoja na namna ya kufundisha matamshi (Musau na Chacha, 2001).

Kuhusu namna ya kufundisha matamshi, Musau na Chacha wanasema kuwa mwalimu anaweza kutumia kinasa sauti kilicho na matamshi sanifu ya Kiswahili. Wanasema kuwa mwalimu anaweza kutumia jozi finyu za maneno ambazo zinatofautiana kwa sauti moja tu na kufanya zoezi la kutofautisha maneno yaliyoko

katika jozi. Aidha, mwalimu anaweza kuwasomea wanafunzi wake sentensi mbili zinazotofautishwa kwa neno moja tu kwenye sauti anayotaka kufundisha. Mfano; **Msasi atafika kesho na mzazi atafika kesho**. Mwalimu anaweza kutumia imla kufunza matamshi na vilevile anaweza kuwaonyesha wanafunzi wake kutamka sauti fulani kwa kurejelea viungo vya utamkaji na jinsi ya kutamka.

Kwa vile lengo kuu la lugha ni kuwasiliana, ufundishaji wa matamshi unaambatana na stadi za kuzungumza. Watafiti hawa walipendekeza mbinu za maigizo, mazungumzo yanayotokana na tarakimu, matumizi ya picha na michoro, pamoja na mijadala kama mbinu mwafaka za kufunza mazungumzo ya Kiswahili. Musau na Chacha (2001) wanahitimisha kwa kusema kuwa ni jukumu la kila mwalimu kuwapa wanafunzi mazoezi ya kutosha. Hata hivyo utafiti huu haukulenga changamoto zinazowakumba wanaojifunza sauti na matamshi ya Kiswahili. Aidha, haukujikita katika ufunzaji wa kiwango cha shule ya upili kama ilivyo utafiti wetu.

King'ei na Musau (2002) walitafiti kuhusu utata wa Kiswahili. Wao walisema kuwa, wazungumzaji wasiotumia matamshi sahihi ya Kiswahili hawaeleweki vizuri kila mara. Wanasema kwamba matatizo ya kimatamshi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili nchini Kenya yana asili kuu ambayo ni athari za lugha ya kwanza. Njia moja inayotumiwa na walimu au wanaisimu kubashiri matatizo waliyo nayo wazungumzaji wa Kiswahili kama L2 ni kulinganisha sauti za lugha ya kwanza na zile za Kiswahili (King'ei na Musau, 2002).

King'ei na Musau (2002) walieleza matatizo ya kimatamshi kwa kulinganisha vitamkwa vya Kiswahili na vile vya lugha za kwanza kama Kinandi, Kijaluo, Kikamba, Kibukusu, Kimaasai na Kisomali. King'ei na Musau (2002), walitazama kuwa sauti nyingi za kukopwa kutoka Kiarabu huwapa matatizo makubwa wazungumzaji wengi. Hii ni kwa sababu baadhi ya sauti hazipatikani katika lugha nyingi za Kenya kama vile Kikuyu, Kikamba miongoni mwa nyingine. Mifano ya sauti hizo ni /th/, /dh/ na /gh/. Walisema kuwa sauti nyingine zinazowatatiza wazungumzaji wengi ni /z/, /j/, /b/ ,/d/. /g/ ,/v./ na /r/.

Tofauti na utafiti wetu, King'ei na Musau (2002), walishughulikia utata wa matamshi ya Kiswahili waziwazi na aina za makosa yenyewe pasi na kujikita katika ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi shuleni. Vile vile King'ei na Musau (2002), walishughulikia matatizo ya kimatamshi kwa kulinganisha vitamkwa vya Kiswahili na zile za lugha za kwanza kama Kinandi, Kijaluo, Kikamba, Kibukusu, Kimaasai na Kisomali tofauti na utafiti wetu uliohusisha walimu na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili katika shule za upili kaunti ya Murang'a Kenya.

Njogu na Nganje (2006) wanasema kuwa silabasi ya Kiswahili imegawanywa kwa stadi nne; kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Wanadai kwamba stadi ya kusikiliza na kuongea ni muhimu kwa mwanafunzi kwani huimarisha usikizaji na uelewaji mzuri wa lugha. Stadi hizi pia humtayarisha mwanafunzi kutamka na

kuyaendeleza maneno ya lugha vizuri. Aidha, stadi hizo zinakusudiwa pia kumpa mwanafunzi ujasiri wa kujieleza bila uoga.

Wanapendekeza mbinu za kufuatwa na mwalimu aliye na wanafunzi ambao wana matatizo ya matamshi (Njogu na Nganje 2006); yaani, kutambua sauti zinazowatatiza, kuwapa mazoezi ya kutamka maneno, kutungia sentensi na kuandika mara kwa mara. Tofauti na utafiti wetu, Njogu na Nganje (2006) walishughulikia vipengele vyote vya ufunzaji Kiswahili kwa ujumla tu wakilenga kuwaandaa wanafunzi wa vyuo vya walimu. Njogu na Nganje (2006) hawakujikita kwa undani katika masuala ya ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili na hivyo utafiti wao kuwa tofauti na wetu.

Kawoya na Ryanga (2010), wanasema kuwa kusikiliza na kuongea kunachukua karibu asilimia 75 ya shughuli za mawasiliano ya kila siku na hivyo kutazama stadi hii kuwa muhimu kwani darasani mafunzo hutegemea sana lugha ya mazungumzo pamoja na kufanikisha juhudi za kufunza msamiati. Wanasema kuwa chanzo cha matatizo ya kusikiliza na kuongea ni pamoja na matamshi mabaya. Mbali na watafiti hawa kuzungumzia matatizo ya kimatamshi kama vile mpishano wa vitamkwa, upachikaji wa vitamkwa, wameshughulikia mbinu za kufunza matamshi ya Kiswahili.

Kawoya na Ryanga (2010) wanasema kuwa ili kufunza matamshi, hatua tatu za kimsingi zinahitaji kufuatwa; yaani kuendeleza upokezi sikizi ambapo mwanafunzi anapewa fursa ya kupokea na kusikia matamshi ya vitamkwa

mbalimbali katika muktadha wa mfululizo wa maneno. Hatua ya pili ni kuendeleza upambanuzi sikizi yaani uwezo wa kuchanganua sauti anazosikia. Hatua ya mwisho ni kuendeleza upambanuzi zungumzi yaani kuona mwanafunzi anatamka maneno kwa kuzingatia matamshi sahihi. Unapofundisha matamshi unaweza kutumia kinasa sauti, au kuwasomea kwa sauti wanafunzi wakisikiliza jinsi maneno mbalimbali yanavyotamkwa na kisha wanajaribu kuiga matamshi hayo. Unaweza pia kuzipitia hatua hizo kwa kutumia jozi finyu za maneno (Kawoya na Ryanga 2010).

Aidha, Kawoya na Ryanga (2010) wameshughulikia mbinu za majadiliano, maigizo, masimulizi, majibizano, picha, michoro na vibonzo kama mbinu mwafaka za kufundisha mazungumzo. Licha ya utafiti wa Kawoya na Ryanga (2010) kukaribiana na utafiti wetu, haukujikita katika ufunzaji wa fonetiki na fonolojia ya Kiswahili katika shule za upili. Aidha, hawakulenga kubainisha changamoto wanazokumbana nazo walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili katika harakati ya kujifunza matamshi ya Kiswahili.

Basi ni bayana kuwa tafiti nyingi za awali zililenga kuonyesha matatizo ya kimatamshi ya Kiswahili na aina za makosa ya kimatamshi. Zile tafiti zilizokaribiana na utafiti wetu nazo hazikushughulikia vipengele vyote kwa undani kama vile ufundishaji wa fonimu za Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Kwa mfano, walioshughulikia mbinu za ufunzaji matamshi ya Kiswahili hawakushughulikia

changamoto halisi zinazokumba ufunzaji matamshi. Aidha, hakuna utafiti wowote uliotathmini yanayofunzwa katika kiwango cha shule za upili kuhusu fonetiki na fonolojia ya Kiswahili nchini Kenya. Hivyo basi, utafiti huu unanuia kuziba pengo hilo lililoachwa na tafiti za awali.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti wetu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya fonolojia zalishi kielelezo cha S.P.E. (*Sound Pattern of English*) iliyoasisiwa na Chomsky na Halle (1968) ili kuchanganua data kuhusu sauti za Kiswahili. Aidha, nadharia ya utabia iliyoasisiwa na Skinner (1957) ilikuwa ya manufaa kwetu hasa katika uchanganuzi wa data inayohusu masuala ya ufundishaji fonetiki na fonolojia ya Kiswahili.

### 1.8.1 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Kielelezo cha S.P.E

Nadharia hii ilianzishwa na Chomsky na Halle katika kitabu chao maarufu *Sound Pattern of English (SPE) (1968).* Mageuzi makubwa katika uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia yalitokea wakati wa uanzishwaji wa nadharia ya fonolojia zalishi ambayo ilielezwa kwa uwazi na ufasaha katika kiunzi ambacho kinajulikana leo kama kuinzi rasmi cha fonolojia zalishi (KRFZ). Kiunzi hiki kilianzishwa na Noam Chomsky na Morris Halle katika kitabu chao *Sound Pattern of English (1968).* Miaka ya 1940 na 1950 huko Ulaya Mashariki na Marekani wanafonolojia walishughulika zaidi na nadharia ya fonimu na jinsi ya kuitambua fonimu.

Kwa mujibu wa Massamba (2011:108) "kiunzi cha fonolojia zalishi kinawakilisha vipengele mbalimbali vya kifonolojia kiulalo unaojulikana kama uwakilishi moza

(uwakilishi mkururo).” Hivyo basi vipamba sauti huchukuliwa kama vijenzi vya vitamkwa. Nadharia hii huchanganua fonolojia vitamkwa na fonolojia arudhi katika lugha za binadamu. Kwa mfano, mkazo katika neno mtoto unamilikiwa na unachukuliwa kuwa ni sifa pambanuzi ya irabu ya silabi ya pili kutoka mwisho.

#### 1.8.1.1 Misingi ya Fonolojia Zalishi Kielelezo cha S.P.E.

Nadharia hii ina misingi ifuatayo:

**Msingi I:** Maumbo na miundo yote ya lugha ya binadamu hutokana na umbo la ndani ambalo hujengeka taratibu katika akili ya msemaji mzawa tangu anapoanza kujifunza lugha akiwa mtoto mdogo mpaka anapopata umilisi kamilifu wa lugha yake.

**Msingi II:** Maumbo na miundo ya maneno tutamkayo katika vinywa vyetu huwakilisha umbo la nje, umbo ambalo kwa kiasi kikubwa huakisi umbo la ndani.

**Msingi III:** Sauti zote zitumikazo katika lugha asilia za binadamu hutokana na mifumo ya mkondohewa ambayo ama inakwenda ndani ya mapafu au inatoka nje ya mapafu ya mzungumzaji. Mkondohewa hudhibitiwa na ala za matamshi. Udhibiti huo unakuwa katika jinsi na mahali pa kutolewa au kuingia hewa mapafuni. Misingi hii inadhihirisha nadharia hii inasisitiza kuwepo umbo ndani na umbo la nje la kipengele chochote cha kifonolojia.

Misingi hii huongoza uchambuzi na uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia. Kwa ujumla misingi hii inaonyesha kuwa mkondohewa kama vile wa mapafu ndiyo chanzo kikuu cha kuzalisha sauti.

#### 1.8.1.2 Mihimili ya Fonolojia Zalishi

Nadharia ya fonolojia zalishi (FZ) ina mihimili minne ambayo kwayo nadharia hii hufanya kazi ya kuchanganua, kuchambua na kuwakilisha vipengele vya kifonolojia.

Nadharia hii ina mihimili ifuatayo;

i) Katika uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia na kifonetiki hatuna budi kutumia sifa ambazo zitaweza kuzitofautisha sauti. Ili kutofautisha sauti, kutumia dhana ya uwilisifa ni muhimu. Hii ina maana kuwa sauti ina sifa fulani [+sifa] au haina sifa hiyo [-sifa]. Sauti hupambanuliwa kwa sifa pambanuzi zake. Kwa mujibu wa nadharia hii vigezo vinavyotumiwa kuteua sifa ni kuangalia chemba inayohusika, namna ya utamkaji na chombo cha sauti husika.

ii) Nadharia hii husisitiza haja ya kuweka wazi sheria na kanuni zilizo rasmi na madhubuti ambazo zinaweza kutumiwa kulikotoa umbo moja hadi kufikia umbo la nje kutoka katika umbo la ndani. Sheria hizi hazina budi kufuatwa kwa utaratibu unaooana na usio badilifu. Jambo linalopewa kipaumbele ni ubainishaji wa kanuni na sheria za muundo wa nje.

iii) Haja ya kuwa na utaratibu rasmi, madhubuti na usio badilifu wa jinsi ya kuzitumia sheria katika kulikotoa umbo la nje kutoka umbo la ndani. Sheria zake ni chache, fupi na zisizogharimu maelezo marefu. Kwa mantiki hiyo, mpangilio rasmi unabidi kuonyesha ni sheria ipi itangulie na ipi ifuate (taz. Massamba, 2011).

iv) Pawepo na sababu zinazoeleza kwa nini maelezo au uchanganuzi fulani wa data tuliyopewa ndio unaonekana kuwa bora zaidi kuliko maelezo au uchanganuzi mwingine wowote unaoweza kutolewa kuhusu data hiyo hiyo.

#### 1.8.1.3 Sifa Pambanuzi za Chomsky na Halle

Chomsky na Halle (1968) walizigawa sifa za sauti za Kiswahili katika makundi matatu makuu: yaani;

(i) Usonoranti (dhidi ya zile zisizo na usonoranti.)

[+sono]: kuwa au kutokuwa na usonoranti.

Sifa hii inajumuisha sauti ambazo wakati wa utamkaji hutokea ughunishaji. Sauti zenye usonoranti ni zile ghuna ilhali zile zisizo na usonoranti si ghuna. Sifa hii hujumuisha irabu zote, vilainisho, nazali na viyeyusho.

(ii) Uvokali (dhidi ya zisizo vokali.)

Sauti zenye uvokali hutolewa bila mkondohewa kubanwa kinywani

iii) Ukonsonanti (dhidi ya zisizo na ukonsonanti.)

[+konso]: kuwa au kutokuwa na ukonsonanti. Hugawa sauti katika makundi makuu mawili; irabu na konsonanti. Sauti zenye ukonsonanti ni zile ambazo hutolewa kwa kuzuilia mkondohewa mahali fulani kinywani.

Chomsky na Halle wanabainisha makundi matatu ya uainishaji wa sifa za sauti, yaani:

a) Sifa za chemba ya mkondohewa

Hizi ni sifa ambazo hutokana na chemba mbalimbali zinazohusika na utamkaji wa sauti. Kuna chemba tano kuu, yaani: chemba ya kongomeo, chemba ya mapafu, chemba ya koo, chemba ya kinywa na chemba ya pua. Kwa kutumia kigezo hiki, aina zifuatazo za sauti hubainishwa:

i) Sauti zenye sifa ya [+ukorona]

ii) Sauti zenye sifa ya [+uanteria]

iii) Sauti zenye sifa ya [juu],[+chini],[+nyuma]

iv) Sauti zenye sifa ya mkao wa mdomo (viringe au tandaze)

b) Sifa za jinsi ya kutamka

Kigezo hiki hubainisha aina zifuatazo za sauti:

i) Sauti zenye sifa ya ufulizwa [+kontnuanti]

ii) Sauti zenye sifa ya [+vizuizi]

iii) Sauti zenye sifa ya mwachilio taratibu [+afriketi)

iv) Sauti zenye sifa ya [+kanze]

c) Sifa ya chanzo

Hizi ni sifa ambazo chanzo chake ni ule msukumo wa hewa kutoka mapafuni ambao hufanywa na ala za matamshi. Zifuatazo ni aina za sauti zinazobainishwa kwa kutumia kigezo hiki:

i) Kuwa au kutokuwa na usilabi [+ sila]

ii) Kuwa au kutokuwa na ukonsonanti [+ konso]

iii) Kuwa au kutokuwa na usooranti [+ sono]

iv) Kuwa au kutokuwa na ukorona [+ koro]

v) Kuwa au kutokuwa na uanteria [+ ante]

vi) Kuwa au kutokuwa na umidomo [+ mido]

vii) Kuwa au kutokuwa na utawanyifu [+ tawa]

viii) Kuwa au kutokuwa na juu [+ juu]

ix) Kuwa au kutokuwa na nyuma[+ nyuma]

x) Kuwa au kutokuwa na chini [+ chini]

xi) Kuwa au kutokuwa na viringe [+ viri ]

xii) Kuwa au kutokuwa na kontinuanti [+ konti]

xiii) Kuwa au kutokuwa na utambaza [+ tamba]

xiv) Kuwa au kutokuwa na unazali [+ naza]

xv) Kuwa au kutokuwa na ustridenti [+ stridenti]

xvi) Kuwa au kutokuwa kaze [+ kaze]

xvii) Kuwa au kutokuwa na ughuna [+ ghuna]

Misingi ya nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. imeongoza uchambuzi na uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia. Aidha mhimili wa nadharia hii unaowakilisha sauti za Kiswahili kwa njia ya uwilisifa imefaa utafiti wetu. Sifa pambanuzi zilizopendekezwa na Chomsky na Halle zimezingatiwa katika uchanganuzi wa data ya yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu fonetiki na fonolojia ya Kiswahili.

Nadharia ya fonolojia zalishi kielelezo cha S.P.E. ilitusaidia kuchanganua data inayohusu masuala yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili kama vile fonimu za Kiswahili, shadda na silabi. Nadharia hii haingeweza kushughulikia suala la ufunzaji wa vipengele vya matamshi ya Kiswahili kwa misingi ya mbinu zinazotumika kufunza pamoja na changamoto zinazokumba ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Hivyo basi nadharia ya utabia ilifidia upungufu huo.

### 1.8.2 Nadharia ya Utabia

Nadharia hii imejengwa katika misingi ya nadharia ya Saikolojia iitwayo Utabia. Waasisi wa nadharia hii kama vile Skinner (1957), walidhamiria kueleza namna tabia inavyojengwa. Waliamini kuwa tabia itadumu ikiwa itaigwa, itarudiwarudiwa, na kutuzwa, lakini tabia isiyorudiwa na isiyotuzwa hufifia. Wanautabia kama vile Skinner (1957) walidhani kuwa jambo analojifundisha mtu mwanzo linaathiri lile analojifundisha baadaye.

Wanautabia walisisitiza mambo yafuatayo katika ufundishaji wao wa lugha:

i) Kukariri na kurudiarudia matamshi mazuri ya vipande vya mazungumzo, miundo ya sentensi na drili za aina aina ili kujenga tabia ya lugha iliyo sahihi au lugha isiyo na makosa na athari za lugha mama.

ii) Tabia nzuri katika kujifundisha lugha ya pili hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi ataelekezwa vizuri kutofanya makosa. Kutokea kwa makosa ni jambo la hatari kwa sababu makosa hayo huenda yakawa tabia. Kwa mujibu wa nadharia hii, makosa yanapaswa kutotuzwa au kuadhibiwa ili yasitokee tena.

iii) Vipengele vya lugha vifundishwe kwa njia ya kusikiza na kuzungumza kwanza kabla ya kuandikwa.

iv) Ufundishaji wa sarufi ya lugha ya pili uendeshwe kwa kukariri tamthilia zilizo na miundo ya kisarufi inayofundishwa.

v) Ufundishaji wa sarufi na vipengele vingine vya lugha usifanywe kwa kuchambua vipengele vya lugha. Mwanzoni wanafunzi wakariri na kurudia na kuiga vipengele hivyo na kuvizoea.

vi) Jukumu la mwanafunzi ni kufuata maagizo, ilhali lile la mwalimu ni muhimu sana kwani ndiye kiongozi wa kila tukio darasani. Hususan, mwalimu anatuza matamshi yaliyo sahihi, miundo ya sentensi pamoja na vipande vya tamthilia vinavyorudiwa na kukaririwa ili tabia ya lugha ijengeke.

Vii) Kujifunza lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha, kama vile fonimu, mofimu na vifungu vya maneno. Kwa sababu hiyo, matamshi yafundishwe mwanzo na sarufi au miundo ya kisarufi baadaye.

Basi kwa vile utafiti wetu ulilenga kuchunguza suala la ufundishaji matamshi ya Kiswahili na changamoto zake, mihimili ya nadharia hii ilikuwa ya manufaa. Kwa mfano, kukariri na kurudiarudia matamshi mazuri, ufunzaji wa fonetiki na fonolojia kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kabla ya kuandika na matamshi kufunzwa mwanzo na vipengele vingine vya kisarufi kufunzwa baadaye ni mihimili iliyoongoza utafiti wetu.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imeeleza mbinu ambazo zilitumiwa kukusanya data na namna mbinu hizo zilitumiwa. Vile vile sehemu hii imeeleza idadi ya sampuli iliyotumiwa na aina za usampulishaji uliotumiwa kuteua sampuli. Mbinu zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa zimeelezwa na vilevile uwasilishaji wa matokeo ya utafiti umeelezwa.

### 1.9.1 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti lilikuwa Kaunti ya Murang'a, Kenya. Shule za upili katika kaunti ya Murang'a hazijafaulu kudhihirisha matokeo mazuri katika mitihani ya kitaifa na hasa katika somo la Kiswahili. Basi tatizo lilistahili kuchunguzwa katika Kaunti ya Murang'a Kenya. Utafiti huu ulinuia kutathmini ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kaunti ya Murang'a.

### 1.9.2 Mbinu za Ukusanyaji Data


Mbinu za utafiti ni mbinu mbalimbali zitakazotumiwa kupata data kutoka kwa walengwa. Utafiti ulikuwa wa aina mbili; utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulibainisha yaliyoandikwa kuhusu mada, maelezo kuhusu misingi ya nadharia na kubainisha yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kwa kurejelea vitabu vya kiada vilivyooidhinishwa na kugharamiwa na serikali ya Kenya..

Utafiti wa nyanjani ulihusisha mbinu za hojaji na mazoezi andishi kama ifuatavyo:

#### 1.9.2.1 Hojaji


Utafiti wa nyanjani ulihusisha hojaji ili kukusanya data kutoka kwa wanafunzi na walimu wao. Hojaji kwa wanafunzi zilisaidia kukusanya data kuhusu mbinu tofauti tofauti wanazotumia kujifunza matamshi ya Kiswahili pamoja na changamoto wanazokumbana nazo. Walimu nao walipewa hojaji kuhusu mbinu za ufunzaji na changamoto pamoja na mielekeo yao na ya wanafunzi wao katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Aidha, tulizingatia vigezo geu vilivyotusaidia kugawa hojaji kwa wahojiwa kama vile kategoria za shule, kidato na kiwango cha shule kama ilivyowasilishwa katika michoro ifuatayo;

**Mchoro 1: Mgao wa hojaji kutegemea kiwango cha Kidato**





Utafiti huu ulihusisha wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha nne pekee kwa kiwango sawa; yaani asilimia hamsini ya wasailiwa walitoka katika kila kidato (cha kwanza na cha nne). Lengo la kusaili wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanafunzi wa kidato cha nne pekee ni kulinganisha umilisi wa mada za matamshi kwa wanafunzi wa kidato cha chini na umilisi wa wanafunzi wa kidato cha juu katika shule za upili.

**Mchoro 2: Mgao wa hojaji kutegemea kiwango cha Kaunti ndogo**





Utafiti huu ulihusisha shule mbili mbili kutoka kila kaunti ndogo zilizoko katika kaunti ya Murang'a. Kaunti ya Murang'a ina kaunti ndogo saba yaani Gatanga, Kandara, Maragua, Kigumo, Mathioya, Kangema na Kiharu. Kaunti ndogo tano zilikuwa na wasailiwa asilimia 14 lakini kaunti za Kiharu na Kangema zilikuwa na wasailiwa asilimia 15 kila kaunti ndogo kwani ni kubwa kuliko kaunti ndogo hizo zingine.

**Mchoro 3: Mgao wa hojaji kutegemea kiwango cha Kategoria ya Shule: kutwa au bweni**





**Mchoro 4: Mgao wa hojaji kutegemea kiwango cha Kategoria ya Shule: wasichana, wavulana au mseto**



Utafiti huu ulihusisha shule za kategoria mbalimbali. Asilimia hamsini ya waliosailiwa walikuwa wanafunzi wa shule za kutwa. Asilimia hamsini walikuwa wanafunzi wa shule za bweni. Aidha utafiti huu ulithibitisha kuwa asilimia 42 ya wanafunzi waliohojiwa walitoka shule za mseto nayo asilimia 29 ilikuwa shule za wasichana pekee na asilimia 29 ilihusisha shule za wavulana pekee. Yaani shule sita kati ya zote kumi na nne zilizohusishwa zilikuwa za mseto nazo shule nne nne zilihusisha wasichana pekee na wavulana pekee mtawalia.

**Mchoro: 5 Mgao wa hojaji kutegemea Kiwango cha Shule: kaunti ndogo, kaunti, kieneo au kitaifa**



Kutokana na mchoro huu, utafiti huu ulihusisha asilimia hamsini ya shule za kiwango cha kaunti ndogo. Aidha, asilimia 28.57 walikuwa wa kiwango cha kaunti. Asilimia 14.29 walikuwa kiwango cha kieneo na asilimia 7.14 walikuwa wa kiwango cha kitaifa.

#### 1.9.2.2 Mazoezi Andishi

Aidha, wanafunzi walipewa mazoezi andishi mifano ya maswali yanayotahiniwa katika mtihani wa kitaifa ili kubainisha kiwango cha umilisi wao kuhusu mada hizi za matamshi ya Kiswahili na changamoto wanazokumbana nazo katika kujibu maswali ya sauti na matamshi ya Kiswahili.

### 1.9.3 Majaribio ya Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti vilifanyiwa majaribio katika shule moja ya upili kutoka eneo la Murang'a ili kubainisha ufaafu wa vifaa hivyo katika ukusanyaji wa data lengwa. Wanafunzi na walimu walipewa hojaji ili kubainisha utata katika kujaza hojaji hizo. Baada ya kufanya majaribio katika Shule ya Upili ya Rwegetha ambayo haikuhusishwa katika utafiti wenyewe, tuligundua kuwa baadhi ya maswali katika hojaji kwa wanafunzi hayakueleweka vizuri kwa wahojiwa. Marekebisho ya vifaa hivyo yalifanywa kabla ya ukusanyaji data ili kuhakikisha uhalali na utegemevu katika ukusanyaji data.

### 1.9.4 Usampulishaji

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), usamplishaji ni hatua ya kuteua idadi ndogo ya walengwa katika mchakato wa utafiti ili kuwatumia kukusanya

data. Sampuli ni sehemu ndogo inayoteuliwa ili kuwakilisha jumuia nzima ya walengwa katika utafiti. Data inayokusanywa kutokana na sampuli ni kiwakilishi cha ukweli kuhusu idadi nzima ya walengwa.

Utafiti huu uliteua sampuli za kimaksudi. Sampuli za kimaksudi huteuliwa kulenga sehemu ya idadi nzima ya walengwa ambayo inajulikana kuwa na habari zinazotafitiwa. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa sampuli za kimaksudi huteuliwa kwa sababu mtafiti anajua kuwa data anayotaka inapatikana kwa watu mahsusi wenye sifa fulani lengwa. Maoni ya Milroy na Gordon (2003) kuwa sampuli ndogo ndiyo mwafaka katika utafiti yatazingatiwa. Shule kumi na nne za upili ziliteuliwa kufanyiwa utafiti. Kaunti ya Murang'a ina kaunti ndogo saba. Kwa kila kaunti ndogo, shule mbili ziliteuliwa. Kategoria zote za shule zilihusishwa katika utafiti yaani shule za wasichana za kutwa, za wavulana, za bweni za kiwango cha kitaifa, za kaunti na za kiwango cha kiwilaya.

Wanafunzi sita, watatu wa kidato cha kwanza na watatu wa kidato cha nne waliteuliwa katika kila shule ili kutathmini uelewa wa sauti na matamshi ya Kiswahili katika kiwango cha chini na katika kiwango cha juu cha shule za upili nchini Kenya. Hii ni kutokana na msingi wa maoni ya Wolfram na Schilling (1998) kuwa katika utafiti wa lugha kila kundi liwakilishwe na angalau watu watano na idadi ya wahojiwa iwe kati ya 48-120. Walimu wawili wawili wa Kiswahili kutoka kila shule walishirikishwa katika kujaza hojaji.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni hatua ya kupanga data iliyokusanywa nyanjani kwa makundi mbalimbali kutegemea malengo ya utafiti. Uchanganuzi wa data uliongozwa na misingi na mhimili wa nadharia ya fonolojia zalishi kielelezo cha S.P.E. ya Noam Chomsky na Halle (1968) ya uwilisifa kuchanganua data kuhusu yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi ya Kiswahili. Data kuhusu ufundishaji wa matamshi ya Kiswahili ilichanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya utabia. Data hii ilichanganuliwa kwa kufuata hatua mbili; data kuhusu mbinu za ufunzaji na data kuhusu changamoto za ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Uchanganuzi wa kitakwimu ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi tarakimu sayansi za kijamii. Mbinu hii hudhihirisha na kuwasilisha matokeo kwa viwango vya kiasilimia.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Hii ni hatua ya kueleza namna data iliyochukuliwa ilivyotokea. Matokeo yamewasilishwa kimaelezo na kijarabati kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Maelezo yametolewa kuhusu yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi, changamoto na mbinu za ufunzaji na ujifunzaji wa mada husika kama vile fonimu za Kiswahili, silabi na shadda. Vile vile, tumetumia michoro duara na majedwali kuwasilisha matokeo ya mbinu na changamoto za ufunzaji wa mada hizi.

### 1.9.7 Uzingatifu wa Maadili

Utafiti huu ulifuata maadili yote ya utafiti. Tulipata kibali kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta, NACOSTI na kwa walimu wakuu wa shule tulizochagua kwa ajili ya utafiti wetu. Watafitiwa walijulishwa sababu ya utafiti na wakatoa habari kwa hiari. Aidha, watafitiwa walihakikishiwa kuwa majibu waliyoyatoa yalikuwa kwa ajili ya utafiti na hayangetumika kwingine kwa sababu nyingine yoyote ile.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imekuwa msingi na utangulizi wa masuala muhimu ambayo yameshughulikiwa katika utafiti huu. Kati ya yale yamegusiwa katika sura hii ni pamoja na usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka, misingi ya kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Masuala haya yote yalikuwa muhimu kwetu kwani yalijenga msingi wa sura zilizofuatia. Sura inayofuata imefafanua dhana za fonetiki na fonolojia kwa utondoti. Sura hii ina umuhimu kwani utafiti huu unahusiana na vipashio hivi vya kimsingi kabisa katika lugha yoyote ile.

# SURA YA PILI

## UFUNZAJI WA MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI

### 2.0 Utangulizi

Ufahamu wa masuala yanayofunzwa kuhusu matamshi na sauti za Kiswahili katika shule za upili ni muhimu katika utafiti huu. Kipengele hiki ni msingi wa sura zilizofuata baadaye. Sura hii imefafanua kwa njia ya kutathmini yale hasa yanayofunzwa katika shule za upili kuhusiana na sauti na matamshi ya Kiswahili kwa kila kidato. Kwa kufanya hivi lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kutathmini masuala yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu sauti za Kiswahili limeshughulikiwa. Hata hivyo, katika kuweka wazi sura hii, tulipitia silabasi ya Kiswahili (K.I.E, 2002) na kubainisha vipengele muhimu vilivyopendekezwa kufunzwa katika shule za upili kuhusiana na matamshi ya Kiswahili. Vile vile tulipitia vitabu teule vya kiada vilivyoidhinishwa na K.I.C.D. *(Kenya Institute of Curriculum Development)* na kugharamiwa na serikali ya Kenya kufunzia somo la Kiswahili nchini Kenya.

Vitabu hivyo ni vifuatavyo; *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018*)*, *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015). Lengo la kupitia vitabu hivi ni kuchunguza yale mapendekezo ya silabasi kuhusiana na ufunzaji wa matamshi kama yanaoana na yale yaliyoandikwa katika vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na K.I.C.D. kufunzia

Kiswahili na hasa mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

Uchanganuzi wa data ya masuala yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili tumeugawa kwa kuzingatia vigezo viwili vikuu. Navyo ni; kigezo cha kuzingatia mahitaji ya silabasi ya Kiswahili (K.I.E, 2002) kuhusiana na ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili kwa kila kidato katika shule za upili. Vile vile tumezingatia kigezo cha kutathmini mada za matamshi ya Kiswahili katika vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na K.I.C.D. na kugharamiwa na serikali ya Kenya kwa kila mwanafunzi na kwa kila kidato kufunzia somo la Kiswahili katika shule za upili.

### 2.1.0 Silabasi ya Kiswahili na Ufunzaji wa Matamshi ya Kiswahili katika Shule za Upili nchini Kenya

Kulingana na Musau na Chacha (2003), silabasi ni mpangilio wa kijumla wa mada zinazotakiwa kufunzwa katika darasa au kidato fulani kwa mwaka mzima katika somo mahsusi. Silabasi humwongoza mwalimu kufahamu kitakachofunzwa. Zaidi ya hayo, silabasi hufafanua malengo ya somo na kutoa vidokezo vya mambo yanayotakikana kufunzwa ili kutimiza malengo hayo. Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa Nchini Kenya (Kenya Institute of Currriculum Development) kwa kifupi K.I.C.D, ndiyo huwa na jukumu la kuandaa na kusambaza mitalaa kwa njia ya silabasi. Utafiti wetu ulibaini kuwa, mafunzo katika silabasi ya Kiswahili, (K.I.E, 2002) yamegawanywa katika sehemu nne kulingana na stadi nne za kujifunza lugha

pamoja na matumizi ya lugha, nazo ni *kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha, kusoma na kuandika.*

Aidha, mada za silabasi hii zimepangwa kulingana na vidato; yaani yale yanayohitaji kufunzwa katika kila kidato na kila stadi. Silabasi yenyewe inapendekeza mwalimu atilie mkazo uwezo wa kuwasiliana kwa kuzingatia stadi za lugha (K.I.E, 2002:27). Utafiti huu basi ulibainisha wazi mada maalum zinazohusiana na sauti na matamshi zilizopendekezwa na silabasi ya Kiswahili kwa mpangilio wa kila kidato na stadi husika.

### 2.1.1 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Kwanza

Baada ya kupitia silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002) tulibaini kuwa, wanafunzi wa kidato cha kwanza wanahitaji kufunzwa mada mbalimbali zinazohusiana na matamshi ya Kiswahili kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali 2.

**Jedwali 2: Mada za matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza**

| Stadi | Yaliyomo |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | Matamshi bora<br>i) shadda<br>ii) kiimbo<br>iii) irabu/vokali- /a/,/e/,/i/,o/,/u/<br>iv) konsonanti<br>/b/,ch//d/,/dh/,/f/,/g/,/gh/,/h/,/j/,/k/,/l/,/m/,/n/,/ng'/,/ny/,/p/,/r/,/s/,/sh//,t/,/th/,/v/,/w/,/y/,/z/<br>v) Ala za sauti/kutamkia<br>vi) Namna ya kutamka na aina za sauti. Mfano, ghuna, sighuna/ hafifu, vipasuo, vikwamizo na kadhalika.<br>vii) Silabi<br>viii) maneno<br>ix) Vitate -mfano, baba, papa<br>x)Vitanza ndimi |
| Sarufi na matumizi ya lugha | sauti: i) irabu/ vokali<br>ii) konsonantianti<br>iii) Mpangilio ilio wa sauti katika silabi na maneno |
| Kusoma | i) Sauti mwambatano<br>ii) Sentensi<br>iii) Kusoma vifungu vya maneno na aya kwa matamshi bora |

Utafiti wetu kama ilivyowasilishwa katika Jedwali 2, umebainisha kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza umetiliwa maanani. Vipengele vya kifonolojia vinafunzwa. Wanafunzi wanafunzwa namna ya kutamka sauti mbalimbali na mahali sauti zinatamkiwa, wanabainisha sauti za Kiswahili yaani irabu na konsonanti na namna zinatamkwa pamoja na mahali zinatamkiwa. Aidha, sifa arudhi kama vile silabi, mkazo na kiimbo vinaelezwa kinaganaga. Wanafunzi wanasoma sentensi na vifungu vya ufahamu kwa sauti na matamshi bora ya Kiswahili. Ilibainika kuwa, katika kidato cha kwanza msingi mzuri wa ufunzaji matamshi ya Kiswahili umewekwa na mada zote zinazofunzwa katika kidato hiki zinalenga mhimili wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. wa uwili sifa. Mfano; kuwa au kutokuwa na ughuna, kuwa au kutokuwa na unazali na kadhalika.

Sauti /b/ ni +ghuna

/p/ ni -ghuna

Ufunzaji wa sauti za Kiswahili katika kidato hiki umepambanuliwa kwa sifa pambanuzi zake na vigezo vya chemba inayohusika, namna ya utamkaji na chombo cha sauti husika. Sifa pambanuzi za chombo zimebainika wazi katika mada hizi kama usonoranti, uvokali, ukonsonanti (konso), sifa za chombo ya mkondohewa, sifa za jinsi ya kutamka kama vile vizuizi, vipasuo, sifa chanzo; mfano sauti zenye sifa ya juu, chini, nyuma, sauti zenye sifa ya mkao wa mdomo (viringe na tandaze), kuwa au kutokuwa na utambaza, kuwa au kutokuwa na unazali, kuwa au kutokuwa na ughuna, kuwa au kutokuwa na usilabi na kadhalika.

### 2.1.2 Mahitaji ya Silabasi kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Pili

Kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili, wanafunzi wa kidato cha pili wanahitaji kufunzwa mada mbalimbali zinazohusiana na matamshi ya Kiswahili kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali 3.

**Jedwali 3: Mada za Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Pili**

| Stadi | Yaliyomo |
|---|---|
| Kusikiliza na kuzungumza | Matamshi bora:<br>i. Silabi tatanishi-pa/ba, sa/sha, la/ra,cha/sha, za/sa, na kadhalika.<br>ii. Sauti tatanishi /d/,/nd/ ,/g/ /ng/, /b/ /mb/ na kadhalika<br>iii. Vitate- kua/kuwa<br>iv. Vitanza ndimi |
| Kusoma | Kusoma kwa sauti:<br>a. Kusoma sauti na maneno tatanishi<br>b. Vitate mfano, kua/kuwa,pua/bua,vua/fua<br>c. Maneno tatanishi yenye sauti mwambatano mfano kidani/ kindani, buni/ mbuni<br>d. Sentensi zenye maana tatanishi<br>e. Vitanza ndimi |

Katika Jedwali 3, ilibainika kuwa silabasi ya Kiswahili imependekeza mada za sauti na matamshi ya Kiswahili kufunzwa chini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza pamoja na kusoma kwa sauti. Utafiti huu uligundua kuwa matamshi bora yalitiliwa uzito katika kidato cha pili. Utamkaji wa sauti tatanishi, silabi tatanishi, maneno tate na kusoma vitanza ndimi kwa sauti na kwa matamshi bora yamependekezwa na silabasi ya Kiswahili. Hata hivyo, ufafanuzi wa sifa za sauti mbalimbali za Kiswahili pamoja na sifa arudhi kama vile shadda, silabi na kiimbo hazijahusishwa katika ufunzaji matamshi kwa wanafunzi wa kidato cha pili.

### 2.1.3 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha tatu

Kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili, wanafunzi wa kidato cha tatu wanahitaji kufunzwa mada mbalimbali zinazohusiana na matamshi ya Kiswahili kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali 4

**Jedwali 4: Mada za Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Tatu**

| Stadi | Yaliyomo |
|---|---|
| Kusoma kwa sauti | i) Kusoma kazi walizotunga kwa sauti<br>ii) Kusoma magazeti wakizingatia tahariri, habari za kimataifa na barua kwa mhariri, ripoti za michezo<br>iii) Kusoma habari na ripoti za runinga na redio<br>iv) kusoma sentensi na kurekebisha makosa |

### 2.1.4 Mahitaji ya Silabasi ya Kiswahili kuhusu Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Nne

Kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili, wanafunzi wa kidato cha nne wanahitaji kufunzwa mada mbalimbali zinazohusiana na matamshi ya Kiswahili kama ilivyoorodheshwa katika Jedwali 5.

**Jedwali 5: Mada za Matamshi ya Kiswahili katika Kidato cha Nne**

| Stadi | Yaliyomo |
|---|---|
| Kusoma kwa sauti | i) Kusoma kazi walizotunga kwa sauti<br>ii) Kusoma vitabu teule<br>iii) Kusoma ripoti za wahariri wa magazeti<br>iv) kusoma matangazo |

Kutokana na Jedwali 4 na Jedwali 5 tuligundua kuwa mada za matamshi ya Kiswahili kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili zimebainika katika stadi ya kusoma pekee. Baada ya kupitia silabasi ya Kiswahili K.I.E. (2002), utafiti wetu ulibaini kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika vidato vya juu, yaani kidato cha tatu na cha nne, umepuuzwa na haujapewa uzito wa kutosha. Mwanafunzi anahitajika kusoma kwa sauti magazeti, matangazo mbalimbali pamoja na habari za kitaifa na za kimataifa. Msingi wa sifa za sauti za Kiswahili haujarejelewa katika vidato vya tatu na vya nne. Masuala ya silabi, shadda na kiimbo hayajazungumziwa katika vidato hivi vya tatu na nne mtawalia.

## 2.2 Mada za Matamshi ya Kiswahili katika Vitabu vya Kiada katika Shule za Upili Nchini Kenya

Baada ya kupitia silabasi ya Kiswahili na kubainisha yale yanahitaji kufunzwa kuhusu mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili na katika kila kidato, kulikuwa na haja ya kupitia vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na kupendekezwa na serikali ya Kenya kufunzia somo la Kiswahili. Lengo la kupitia vitabu hivi ni kubaini kama yale yaliyopendekezwa na silabasi yamezingatiwa katika uandishi wa vitabu vya kiada. Vile vile kuhakiki yanayofunzwa kwa mujibu wa vitabu vya kiada, kulichangia kutimiza lengo letu la kwanza la kutathmini yanayofunzwa kuhusu mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Vitabu teule vilivyopitiwa ni vinne; yaani kitabu kimoja kwa kila kidato. Navyo ni: *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015).

### 2.2.1 *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018)

Baada ya kupitia kitabu hiki tuling'amua kwamba wanafunzi walipewa mafunzo mengi kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza. Tulitambua kuwa mafunzo mengi yalihusishwa katika stadi ya kusikiliza na kuzungumza kama yalivyo mahitaji ya silabasi. Katika stadi hii, wanafunzi wanafunzwa sauti za Kiswahili kwa jumla katika sura za kwanza sita za kitabu hiki. Maana ya sauti, mgawanyo wa sauti za wanadamu, yaani irabu na konsonanti, muainisho wa irabu zote za Kiswahili na sifa zake bainifu zilibainika. Mhimili wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E ya Chomsky

na Halle (1968) ya uwilisifa ilibainika. Mfano; kuwa au kutokuwa na uviringe na kadhalika. Vigezo vitatu vya kubainisha irabu za Kiswahili vilibainika kama vile, mkao wa mdomo- mdomo- kuwa viringe au kutokuwa viringe, kigezo cha sehemu ya ulimi inayohusishwa na utamkaji wa irabu-sehemu ya mbele, nyuma na sehemu ya juu. Aidha kigezo cha mwinuko wa ulimi yaani ulimi kuinuka juu, kuwa kati na kuwa chini.

Sauti 26 za konsonanti za Kiswahili zimebainishwa katika u.k. 2, matamshi yake na mifano ya maneno yametolewa. Vilevile ala 12 za matamshi kama vile midomo, meno, ufizi, chemba cha pua, kidakatonge, miongoni mwa nyingine zinafunzwa kwa mujibu wa kitabu hiki. Tuligundua kuwa sifa pambanuzi za Chomsky na Halle (1968) zilizingatiwa katika kuainisha sauti na konsonanti za Kiswahili. Mfano; sifa ya usonoranti (dhidi ya zile zisiso na usonoranti.) yaani sauti kuwa ghuna au kutokuwa ghuna imebainishwa (taz. uk.22), sifa za jinsi ya kutamka kama vile; vipasuo, vikwamizwa, vizuiwa-kwamizwa, kitambaza, kimadende, nazali na viyeyusho vinafunzwa. (taz. uk. 22). Vile vile sifa ya mahali pa kutamkia kama vile midomoni, midomo meno, meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini na koromeo imetumiwa kuainisha konsonanti mbalimbali za Kiswahili.

Katika kidato cha kwanza, suala la matamshi bora limetiliwa uzito kupitia utamkaji wa jozi za maneno tatanishi pamoja na vitanza ndimi tofauti tofauti (uk 23). Mazoezi ya utamkaji sahihi wa vitate kama vile; apa na hapa, ama na hama, aya na haya miongoni mwa vitate vingine vinafunzwa.

Ufunzaji wa sifa arudhi haujaachwa nyuma katika kidato cha kwanza. Mada za silabi, maana ya silabi na miundo ya silabi za Kiswahili ilibainika kufunzwa. Kiimbo na mchango wake katika kuibua dhamira za sentensi mbalimbali, yaani sentensi amrishi, sentensi hisishi miongoni mwa nyingine zimebainishwa. (taz.uk 10). Shadda au mkazo katika utamkaji wa maneno ya Kiswahili imeangaziwa na msisitizo wa shadda kuwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa maneno ya Kiswahili umebainika.

*Uhondo wa Kiswahili kitabu cha* wanafunzi kidato cha kwanza kina mpangilio wa sura 21. Mafunzo ya sauti na matamshi ya Kiswahili yamerundikwa katika sura za kwanza 6 kupitia stadi tatu za ufunzaji yaani kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha pamoja na stadi ya kusoma kwa sauti. Mengi yanayohusiana na matamshi ya Kiswahili yamebainika katika stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Utafiti wetu ulibaini kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza umepewa kipaumbele ikilinganishwa na vidato vilivyofuata. Aidha, utafiti huu ulibaini uwepo wa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi kuhusiana na vipengele vya mada za matamshi ya Kiswahili katika kitabu hiki.

### 2.2.2 *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018)

*Kiswahili Kitukuzwe kitabu cha* wanafunzi kidato cha pili, kimebainika kuendeleza mada za matamshi za Kiswahili yaliyofunzwa katika kidato cha kwanza. Baada ya kupitia kitabu hiki, tulibaini kuwa suala la matamshi bora limeshughulikiwa katika sura za kwanza 12 kwa jumla ya sura zote 21 chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Wanafunzi wamepewa mazoezi ya kutamka jozi mbalimbali za sauti tata, silabi

tatanishi, maneno tata na kusoma vitanza ndimi kwa matamshi bora mfano, utamkaji wa sauti na maneno tata yanayohusiana na sauti /b/ na /mb/ (uk1), silabi tatanishi /la/ na/ ra/ (uk13), sauti tatanishi /g/ na /ng/ (uk 23) na kadhalika. Aidha, tulibaini kuwa yale yaliyoandikwa katika kitabu hiki yanaoana na mahitaji ya silabasi kuhusiana na ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Hata hivyo, sifa arudhi hazijabainika katika kitabu hiki. Tulibaini kuwa kupitia mada za matamshi katika kitabu hiki wanafunzi wataweza kuendeleza umilisi wao wa konsonanti za Kiswahili na sifa bainifu za konsonanti na kupuuza ufunzaji wa sifa bainifu za irabu za Kiswahili na sifa arudhi kama silabi, shadda na kiimbo.

### 2.2.3 *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018)

Kutokana na uhakiki wetu wa *Kiswahili Kitukuzwe kitabu cha* wanafunzi kidato cha tatu, tulibaini kuwa kitabu hiki kina mpangilio wa jumla ya sura 22. Kati ya sura hizi, sura za kwanza 3 pekee ndizo zimehusishwa na ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Mada hizi zimebainika kuwa chini ya stadi moja pekee yaani stadi ya kusoma kwa sauti. Wanafunzi wanahitaji kusoma tahariri, barua kwa mhariri na habari za kitaifa na za kimataifa kwa matamshi bora. Mfano; kusoma habari za kitaifa na kimataifa (uk 13), kusoma barua kwa mhariri (uk28) na kadhalika. Utafiti huu uliweza kung'amua kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili haujatiliwa uzito katika kidato cha tatu kama ilivyo katika kidato cha kwanza na cha pili. Mazoezi ya kukoleza umilisi wa yaliyofunzwa kuhusu sifa bainifu za sauti za Kiswahili na sifa arudhi hayakubainika katika kidato cha tatu. Hata hivyo, malengo ya silabasi kuhusu ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tatu yalitimizwa katika uandishi wa kitabu hiki ipasavyo.

### 2.2.4 *Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015)

Baada ya kupitia kitabu hiki cha *Kiswahili Fasaha kwa kidato cha* nne, hatukubaini mada zozote zinazohusiana na matamshi ya Kiswahili. Yanayokaribia matamshi ya Kiswahili ni mada za kusoma kwa kina ambazo si lazima zihusishe matamshi bora. Hata hivyo, katika sura ya 10 ya kitabu hiki kuna mazoezi ya marudio kwa wanafunzi ambapo ni maswali mawili pekee yalibainika kuhusiana moja kwa moja na mada za sauti na matamshi ya Kiswahili yaani swali 1 a, 1 b na swali la 3 (tz. uk 111). Silabasi ya Kiswahili ilipendekeza usomaji kwa sauti wa matangazo na ripoti za wahariri wa magazeti lakini hatukubaini yoyote yanayohusiana na mada hizi katika kitabu hiki. Utafiti huu uligundua udhaifu wa kitabu hiki katika kutayarisha watahiniwa na kukuza umilisi wao kuhusu mada za sauti na matamshi ya Kiswahili.

Utafiti huu uligundua kwamba ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza na cha pili umetiliwa maanani. Katika kidato cha kwanza, vipengele vya kifonolojia na hata vya kifonetiki vinafunzwa. Katika fonetiki wanafunzi wanafunzwa namna ya kutamka sauti mbalimbali na mahali sauti zinatamkiwa. Katika fonolojia, wanafunzi wanabainisha sauti za Kiswahili yaani irabu na konsonanti na namna zinatamkwa pamoja na mahali zinatamkiwa. Aidha, sifa arudhi kama vile silabi, mkazo na kiimbo vinaelezwa kinaganaga. Utafiti huu ulibaini kuwa msingi mzuri wa ufunzaji matamshi ya Kiswahili umewekwa na mada zote zinazofunzwa katika kidato hiki cha kwanza zinalenga mhimili wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. wa uwili sifa.

Katika kidato cha pili ilibainika kuwa kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili, mada za sauti na matamshi ya Kiswahili zilifunzwa chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza pamoja na kusoma kwa sauti. Utafiti wetu uligundua kuwa matamshi bora yalitiliwa uzito katika kidato hiki. Utamkaji wa sauti tatanishi, silabi tatanishi, maneno tata na kusoma vitanza ndimi kwa sauti kulifunzwa. Hata hivyo, upambanuzi wa sifa za sauti mbalimbali za Kiswahili pamoja na sifa arudhi kama shadda, silabi na kiimbo hazikuendelezwa katika kidato cha pili.

Utafiti huu ulibaini kuwa katika vidato vya juu, yaani kidato cha tatu na cha nne, mada za sauti na matamshi ya Kiswahili hazikutiliwa maanani sana kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili. Katika vidato hivi, ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili umehusishwa katika stadi ya kusoma pekee. Mwanafunzi anahitajika kusoma kwa sauti magazeti, matangazo mbalimbali pamoja na habari za kitaifa na za kimataifa. Msingi wa sifa za sauti za Kiswahili haurejelewi katika vidato vya tatu na vya nne. Masuala ya shadda, silabi na kiimbo haujazungumziwa katika vidato hivi.

Utafiti huu ulipitia vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na kupendekezwa na serikali ya Kenya kufunzia somo la Kiswahili. Lengo la kupitia vitabu hivi lilikuwa kubaini kama yale yaliyopendekezwa na silabasi yanazingatiwa katika uandishi wa vitabu vya kiada. Baada ya kupitia vitabu hivi tuligundua kuwa yaliyomo katika vitabu hivi yalioana kabisa na matarajio ya silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002) katika ufunzaji wa mada za matamshi ya Kiswahili isipokuwa katika *Kiswahili Fasaha kidato cha nne* ambacho hatukubaini chochote kinachohusiana na mada za matamshi ya Kiswahili.

*Uhondo wa Kiswahili Kitabu cha Wanafunzi Kidato cha Kwanza* kina mpangilio wa sura ishirini na moja. Mafunzo ya sauti na matamshi yamehusishwa katika sura za kwanza sita kupitia stadi tatu za ufunzaji yaani kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha pamoja na stadi ya kusoma kwa sauti. Katika kidato cha pili, tulibaini kuwa suala la matamshi ya Kiswahili lilishughulikiwa katika sura za kwanza kumi na mbili kwa jumla ya sura zote ishirini na moja chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Katika kidato cha tatu, ni sura tatu pekee katika jumla ya sura ishirini na mbili zilizohusisha ufunzaji matamshi ya Kiswahili chini ya stadi ya kusoma kwa sauti. Katika kidato cha nne, hatukubaini mada zozote zilizohusiana na matamshi ya Kiswahili.

Utafiti huu basi uligundua kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili umetiliwa uzito katika vidato vya chini na kupuuzwa katika vidato vya juu. Mazoezi ya kukoleza umilisi wa mada za matamshi katika vidato vya juu haukudhihirika. Tuligundua udhaifu huu kutokana na uchanganuzi wa data yetu ya yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili kwa mujibu wa kitabu cha *Kiswahili Fasaha kwa Wanafunzi wa Kidato cha Nne* katika kutayarisha watahiniwa na kukuza umilisi wao kuhusu mada za sauti na matamshi ya Kiswahili.

Katika kidato cha kwanza na cha pili, stadi za kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha pamoja na kusoma kwa sauti vilitumika katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine katika vidato vya juu hakuna maendeleo ya mada zilizofunzwa awali. Stadi moja tu yaani ile ya kusoma kwa sauti ndiyo tu

ilihusishwa katika vidato vya juu. Ni dhahiri kuwa uzoefu wa kutosha wa mada za matamshi haupo katika silabasi ya Kiswahili kutoka kidato kimoja hadi kiingine. Utafiti huu ulikisia kuwa hii ndiyo sababu ya wanafunzi kukosa ukomavu wa kimatamshi pindi wanavyopanda katika vidato vya juu.

**2.3. Hitimisho**

Sura hii imetathmini kwa kina yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Silabasi ya Kiswahili na vitabu vya kiada vinavyotumiwa kufunzia Kiswahili katika shule za upili zilipitiwa. Utafiti huu ulibainisha kuwa ufunzaji wa mada za matamshi ya Kiswahili zimetiliwa maanani sana katika vidato vya chini, yaani katika kidato cha kwanza na cha pili. Stadi za kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matamshi ya lugha pamoja na kusoma kwa sauti zilihusishwa katika ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, katika vidato vya juu hakuna maendeleo ya mada zilizofunzwa awali. Stadi moja tu yaani ile ya kusoma kwa sauti ndiyo tu ilihusishwa katika kidato cha pili na cha tatu. Huenda hii ikawa sababu ya wanafunzi kukosa ukomavu wa kimatamshi pindi wanavyopanda katika vidato vya juu.

Hili lilidhihirishwa na uhakiki wa vitabu vya kiada na hasa vile vilivyoidhinishwa na kugharamiwa na serikali ya Kenya katika kila kidato yaani; *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwaza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015). Yaliyomo katika vitabu

hivi teule yalioana kabisa na matarajio ya silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002) katika ufunzaji wa mada za matamshi isipokuwa katika *Kiswahili Fasaha kidato cha nne* ambacho baada ya kupitia kitabu hicho hatukubaini chochote kinachohusiana na mada za matamshi ya Kiswahili.

Aidha, mhimili wa uwili sifa wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. ulibainika wazi katika ufunzaji wa mada za matamshi. Sifa pambanuzi za Chomsky na Halle (1968), zilibainika kutumika katika uanishaji wa sifa bainifu za sauti za Kiswahili yaani konsonanti na irabu. Basi kwa kupitia sura hii lengo la kwanza la utafiti wetu liliafikiwa kwani tumeeleza wazi yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi ya Kiswahili kwa kupitia silabasi ya Kiswahili na vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa kufunzia Kiswahili katika shule za upili.

Sura inayofuata imeshughulikia uchanganuzi wa data ya mbinu za ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Kupitia sura hii lengo la pili la utafiti huu limeafikiwa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imehusisha uchanganuzi wa data ya mbinu za ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Data hii ilichanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya utabia ya Skinner (1957). Data hiyo ilitokana na hojaji kwa walimu na hojaji kwa wanafunzi wasailiwa wa kidato cha kwanza na cha nne katika shule teule za kauti ya Murang'a. Tulitumia mtindo wa uchanganuzi wa tarakilishi wa uchanganuzi tarakimu sayansi za jamii (S.P.S.S.). Mtindo huu huchunguza kategoria za uchanganuzi na kutathmini idadi ya wasailiwa pamoja na asilimia za matukio, asilimia hubainishwa kwa vigezo viwili; yaani asilimia matukio na asilimia jumla.

## 3.1 Hojaji kwa walimu

Kutokana na hojaji kwa walimu kuhusu zile mbinu wanazotumia kufunza mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili, tulibaini kuwa walimu wanatumia mbinu mbalimbali kama ifuatavyo; kutamka sauti mbalimbali, kusikiliza na kuzungumza kwa sauti, kusoma vifungu, michoro ya mahali pa kutamkia sauti, kufanya mazoezi yanayohusu sauti na matumizi ya vipaza sauti (sauti za matamshi bora yaliyorekodiwa.)

### 3.2 Hojaji kwa wanafunzi

Hojaji hii ilitusaidia kuzoa habari muhimu za uchanganuzi wa data kuhusu mbinu wanazotumia wanafunzi kujifunza matamshi ya Kiswahili. Baada ya kuwahoji wahojiwa tulibaini kuwa wao walitumia mbinu mbalimbali za kujifunza sauti za Kiswahili kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 6: Mbinu za kujifunza sauti za Kiswahili**

| Mbinu | Ndio (Idadi marudio) | Asilimia | La (idadi) | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Ukariri | 61 | 72.6 | 23 | 27.38 |
| Vipasa sauti | 32 | 38.09 | 52 | 61.9 |
| Maigizo | 60 | 71.43 | 24 | 28.57 |
| Chati | 31 | 36.90 | 53 | 63.09 |
| Imla | 53 | 63.09 | 31 | 36.90 |
| Kusoma vifungu | 80 | 95.24 | 04 | 4.76 |
| mazungumzo /majibizano | 70 | 83.33 | 14 | 16.67 |
| Mijadala | 61 | 72.62 | 23 | 27.38 |
| Masimulizi | 66 | 78.57 | 18 | 21.43 |
| Michoro/picha/vibonzo | 53 | 63.09 | 31 | 36.90 |
| Jozi mlinganuo finyu | 07 | 8.33 | 77 | 91.67 |

Kuhusu mbinu za kujifunza sauti za Kiswahili, wanafunzi asilimia 72.6 walithibitisha kutumia mbinu ya ukariri nayo asilimia 27.38 haitumii mbinu ya uradidi. Asilimia 38.09 ilikubali kutumia vinasa sauti lakini asilimia kubwa (asilimia 61.9) haitumii vinasa sauti. Asilimia 71.43 ilidhihirisha kutumia mbinu ya maigizo lakini asilimia 28.57 haitumii maigizo. Asilimia 31 ya wanafunzi wasailiwa ilithibitisha kutumia chati katika ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili ilhali asilimia 53 ya wanafunzi wahojiwa hawatumii chati. Mbinu ya imla ilibainika kutumiwa na asilimia 63.09 ya wanafunzi na asilimia 36.90 haitumii imla kama mbinu ya kujifunza matamshi ya Kiswahili. Mbinu ya kusoma vifungu mbalimbali ilidhihirika kutumiwa na asilimia kubwa (asilimia 95.24) lakini ni asilimia 4.76 tu ambayo haitumii mbinu ya kusoma vifungu. Mazungumzo na majibizano yalitumiwa na asilimia 83.33 ya wanafunzi nayo asilimia 16.67 haikutumia mbinu hii. Mbinu ya mijadala ilitumiwa na asilimia 72.62 ya wanafunzi wasailiwa nayo asilimia 27.38 haikutumia mbinu hii.

Asilimia 78.57 ilithibitisha kutumia mbinu ya masimulizi lakini asilimia 21.43 haikutumia masimulizi. Mbinu ya michoro, picha na vibonzo ilidhihirika kutumiwa na asilimia 63.09 ya wasailiwa ilhali asilimia 36.90 haikutumia mbinu ya michoro na picha. Mwisho mbinu ya jozi mlinganuofinyu ulitumiwa na wanafunzi wachache tu (asilimia 8.33) lakini asilimia kubwa (asilimia 91.67) haikutumia mbinu hii ya jozi mlinganuo finyu kujifunza sauti na matamshi ya Kiswahili.

Utafiti huu uligundua kwamba walimu wanaofunza Kiswahili na mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili ni walimu waliohitimu vizuri kimasomo. Asilimia 77.8 ya walimu waliohojiwa wana shahada ya kwanza. Asilimia 11.1 ya walimu waliosalia wana shahada ya uzamili.

Mbinu za ufunzaji matamshi zilibainika kuwa nyingi. Baadhi ya mbinu tulizongundua zinatumiwa na walimu kufunzia matamshi ni kama: kutamka sauti mbalimbali, kusikiliza na kuzungumza, kusoma vifungu, kutumia michoro, mbinu ya mazoezi ya mara kwa mara yanayohusu sauti na matumizi ya vinasa sauti (sauti za matamshi zilizorekodiwa).

Aidha, tulingundua kuwa wanafunzi hutumia mbinu mbalimbali kujifunza sauti na matamshi ya Kiswahili. Mbinu za ukariri, maigizo, imla, kusoma vifungu, mazungumzo, mijadala, masimulizi na michoro na picha ilidhihirika kutumika na zaidi ya asilimia hamsini ya wanafunzi wasailiwa.

Mbinu iliyotumika zaidi na wanafunzi kujifunza matamshi ya Kiswahili ni mbinu ya kusoma vifungu kwa sauti (asilimia 95.24). Hata hivyo tulibaini kuwa mbinu ya matumizi ya chati, vinasa sauti na ile ya jozi mlinganuo funyu ilitumika na wanafunzi wachache. Tulikisia kuwa mbinu hizi zilikosa kutumika kwa wingi kutokana na ukosefu au uhaba wa vifaa vya kurekodia sauti, chati zenyewe na kalamu za kuchora chati.

Utafiti wetu ulibaini kuwa katika data iliyohusu mbinu za ufunzaji matamshi, mihimili ya nadharia ya utabia ya Skinner (1957) ilizingatiwa. Mbinu za ufunzaji

matamshi zilizogunduliwa na utafiti huu zilioana na mawazo ya wanautabia waliosisitiza ufundishaji wa lugha kuzingatia ukariri wa matamshi mazuri. Ufundishaji wa matamshi kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kwanza kabla ya stadi zingine na mada za matamshi kufundishwa mwanzo na sarufi na miundo yake kufunzwa baadaye. Mihimili hii ya utabia ulidhihirika katika matokeo ya mbinu za ufundishaji matamshi ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, swali la pili la utafiti huu liliweza kujibiwa ilivyokusudiwa.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imechunguza mbinu zinazohusiana na ufunzaji matamshi kwa wanafunzi wa shule za upili. Uchunguzi huu ulitokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu iliyokusanywa kutoka kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanafunzi wa kidato cha nne katika shule za upili kaunti ya Murang'a Kenya. Data hiyo ilihusu vipengele viwili maalum, hojaji kwa wanafunzi na hojaji kwa walimu. Tumetalii na kufafanua data hiyo. Sura inayofuata imeshughulikia uchanganuzi wa data ya changamoto zinazowakumba walimu na wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya.

# SURA YA NNE

# CHANGAMOTO ZA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imehusisha uchanganuzi wa data ya changamoto za ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Data iliyoibuliwa katika utafiti huu ilihusisha mihimili ya nadharia ya utabia ya Skinner (1957). Data hiyo ilihusisha usaili wa walimu, hojaji kwa wanafunzi pamoja na zoezi kwa wanafunzi wasailiwa wa kidato cha kwanza na kidato cha nne, katika shule teule za kaunti ya Murang'a. Tulitumia mtindo wa uchanganuzi tarakilishi wa tarakimu sayansi za jamii (S.P.S.S). Mtindo huu huchunguza kategoria za uchanganuzi na kutathmini idadi ya wasailiwa pamoja na asilimia za matukio, asilimia hubainishwa kwa vigezo viwili; yaani asilimia matukio na asilimia jumla.

### 4.1.0 Hojaji kwa walimu

Tuliwahoji walimu kupata habari muhimu kuhusu changamoto wanazokumbana nazo katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili kama ifuatavyo;

### 4.1.1 Kiwango cha Elimu

Katika shule zote zilizotembelewa, walimu waliohusika katika kufunza Kiswahili katika kidato cha kwanza na cha nne walihojiwa. Shule moja ilikuwa na mwalimu mmoja tu. Walimu ishirini na saba walihusishwa katika kiwango hiki cha uchanganuzi. Matokeo kuhusu kiwango chao cha elimu yalikuwa kama yafuatayo;

**Jedwali 7: Kiwango cha Elimu**

| Kiwango | Idadi maidadi marudio | AsilimiaAsilimia |
|---|---|---|
| Uzamili | 3 | 11.1 |
| Shahada ya kwanza | 21 | 77.8 |
| Stashahada | 3 | 11.1 |
| Nyinginezo | 0 | 00 |
| Jumla | 27 | 100 |

Hapa ilidhihirika kuwa asilimia kumi na moja nukta moja ya walimu wa Kiswahili katika kaunti ya Murang'a wana shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Asilimia sabini na saba nukta saba ya walimu walibainika kuwa na shahada ya kwanza. Walimu watatu kati ya hao ishirini na saba walikuwa na stashahada katika ualimu. Kiwango hiki kilifasiriwa kama asilimia kumi na moja nukta moja. Hakuna mwalimu aliyebainika kuwa na kiwango kingine cha elimu. Matokeo haya yalilenga kubaini kana kwamba kiwango cha elimu cha walimu wa Kiswahili ni changamoto katika ufunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za upili. Tuligundua kuwa kiwango cha elimu hakiathiri ufunzaji matamshi ya Kiswahili kwani walimu wote waliohojiwa walihitimu kufunza shule za upili nchini Kenya.

### 4.1.2 Tajriba ya Ufunzaji Kimiaka

Kusudi la tathmini hii lilikuwa kubainisha tajriba ya walimu ya ufunzaji wa Kiswahili katika shule za upili na kubaini kama tajriba ya ufunzaji kimiaka ni

changamoto katika ufunzaji matamshi au la kama ilivyowasilishwa katika Jedwali 8.

**Jedwali 8: Tajriba ya Ufunzaji Kimiaka**

| Miaka | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 1----5 | 10 | 37.05 |
| 5----10 | 8 | 29.63 |
| 10-----15 | 2 | 7.41 |
| 20 na zaidi | 7 | 25.9 |
| Jumla | 27 | 100 |

Kutokana na Jedwali 8, ilibainika kuwa asilimia thelathini na saba ya walimu wana tajriba ya kati ya mwaka mmoja hadi mitano. Asilimia 29 walikuwa na tajriba ya miaka 5-10. Asilimia saba walikuwa na kati ya miaka 10-15. Aidha, asilimia 25 walikuwa na tajriba ya miaka ishirini na zaidi. Walimu wengi walibainika kuwa na tajriba fupi katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Hii huenda ikawa changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili sababu ya kukosa uzoefu wa kutosha wa kufunza mada hizi.

### 4.1.3 Mwelekeo kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili

Kiwango hiki cha uchanganuzi kilikusudia kuchunguza mwelekeo wa mwalimu kuhusu ufunzaji matamshi ya Kiswahili ili kutathmini kama mwelekeo wa mwalimu ni changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili.

**Jedwali 9: Mwelekeo kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili**

| Mwelekeo wa mwalimu | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Napenda sana | 11 | 40.74 |
| Napenda kiasi | 13 | 48.15 |
| Sipendi | 2 | 7.41 |
| Sina uhakika | 1 | 3.70 |
| Jumla | 27 | 100 |

Matokeo kama yalivyowasilishwa katika Jedwali 9 yalidhihirisha kuwa asilimia 40.74 ya walimu walithibitisha kuwa wanapenda sana somo la matamshi ya Kiswahili. Asilimia 48.15 ya walimu waliohojiwa walikiri kuwa wanapenda kiasi tu ufunzaji wa mada za matamshi ya Kiswahili ilhali walimu wawili kati ya wote 27 walikubali hawapendi somo la matamshi ya Kiswahili. Mwalimu mmoja alikiri hana uhakika kuhusu mwelekeo wake wa ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Data hii ilidhihirisha kuwa mielekeo ya walimu ni changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili.

### 4.1.4 Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili

Hapa tulihoji walimu kuhusu mielekeo ya wanafunzi wao kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Lengo la kuhoji kipengee hiki ni kuchunguza iwapo mielekeo ya wanafunzi ni changamoto ya ufunzaji matamshi au la.

**Jedwali 10: Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Ufunzaji Matamshi ya Kiswahili**

| Mielekeo ya wanafunzi | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Wanalichukulia gumu | 6 | 22.22 |
| Wanalichukulia kwa mzaha | 3 | 3.27 |
| Wanalipenda sana | 4 | 14.81 |
| Wanaopenda kiasi | 6 | 22.22 |
| Wanaopenda linapofunzwa | 5 | 18.5 |
| Wasiopenda | 3 | 13.27 |
| Jumla | 27 | 100 |

Walimu wengi walibaini kuwa wanafunzi wengi wanapenda somo wakati linafunzwa lakini wanapata ugumu kujibu maswali. Aidha, kunao waliodai kuwa wanafunzi wao hawapendi somo lenyewe. Asilimia 22 walidai kuwa wanafunzi walipenda somo la matamshi kiasi. Nayo asilimia 14.8 wanapenda somo la matamshi. Wanafunzi wengine na wale wengi waliripotiwa kuchukulia somo la matamshi kwa mzaha. Hivyo basi mielekeo ya wanafunziilibainika kuwa changamoto kubwa katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

### 4.1.5 Changamoto nyingine zinazoathiri Ufunzaji wa Matamshi ya Kiswahili

Tathmini hili lilienga kubaini changamoto nyingine zinazoathiri walimu katika ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi wetu kuhusu changamoto zenyewe ni kama yalivyoonyeshwa kaika Jedwali 11.

**Jedwali 11: Changamoto zinazoathiri Ufunzaji wa Matamshi ya Kiswahili**

| Changamoto | **Ndio** | Asilimia | **La** | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi Kuathiriwa na lugha ya kwanza | 27 | 100% | 0 | 0 |
| Athari za sheng’ | 27 | 100 | 0 | 00 |
| Athari za lugha ya kigeni | 10 | 37.01 | 17 | 62.96 |
| Mwalimu kuathiriwa na lugha ya kwanza | 8 | 29.63 | 19 | 70.37 |
| Ukosefu wa vitabu maalum | 9 | 33.33 | 18 | 66.67 |
| Ukosefu wa vifaa vya kufunzia | 22 | 81.48 | 05 | 18.52 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Wanafunzi kukosa msingi bora | 23 | 85.16 | 04 | 14.81 |
| Utayarishaji mbaya wa walimu | 11 | 40.74 | 16 | 59.26 |
| Vipindi vichache katika lugha ya Kiswahili | 20 | 74.0781 | 07 | 25.95 |
| Somo la sauti kupangwa kama sura ya 1 kidato cha kwanza | 15 | 55.56 | 12 | 44.44 |

Kama inavyodhihirika kutokana na jedwali hili, walimu wa Kiswahili wanakumbwa na changamoto mbalimbali katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Walimu wote ishirini na saba walikiri kuwa wanafunzi wao waliathiriwa na luhga zao za kwanza na kijilugha cha sheng'. Asilimia thelathini na saba walikubali kuwa wanafunzi wao waliathiriwa na lugha za kigeni. Asilimia sitini na mbili wakadai kwamba wanafunzi wao hawakuathiriwa na lugha za kigeni.

Asilimia 29.63 walikubali kuwa wao wenyewe waliathiriwa na lugha zao za kwanza. Asilimia 70.37 hawakuathiriwa na lugha zao za kwanza. Asilimia 33.33 waliathiriwa na changamoto ya ukosefu wa vitabu maalum vinavyohusisha matamshi ya Kiswahili lakini asilimia 66.67 hawakuathiriwa na ukosefu wa vitabu maalum. Asilimia 81.48 waliathiriwa na ukosefu wa vifaa vya kufunzia sauti nayo asilimia 18.52 hawakuathiriwa na ukosefu wa vifaa maalum vya kufunzia matamshi ya Kiswahili kama vile vinasa sauti, tepu rekoda na projekta. Asilimia 85.16 ya walimu waliohojiwa walikubali kuwa wanafunzi wao wamekosa msingi bora wa matamshi ya Kiswahili katika madarasa ya chini hasa shule za msingi. Ni asilimia 14.81 waliokiri kuwa wanafunzi wao wana msingi bora wa matamshi ya Kiswahili.

Asilimia 40.74 ya walimu waliosailiwa walikiri kuwa utayarishaji wao wa kufunza matamshi ya Kiswahili katika vyuo vya walimu na vyuo vikuu ulikuwa na dosari lakini asilimia 59.26 walikubali kuwa utayarishaji wao wa kufunza matamshi ya Kiswahili ulikuwa mwafaka. Aidha, asilimia 74.07 walithibitisha kuwa vipindi vichache katika lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na lugha ya Kingereza ni changamoto kubwa kwa walimu. Asilimia 25.95 hawakuona vipindi vichache vya Kiswahili kama changamoto kwao. Asilimia 55.56 waliona somo la sauti za Kiswahili kupangwa kama sura ya kwanza katika kidato cha kwanza kama changamoto lakini asilimia 44.44 hawakuwa na shida yoyote kuhusu upangaji wa sauti za Kiswahili katika sura ya kwanza katika silabasi ya Kiswahili kidato cha kwanza.

### 4.1.6 Hatua Faafu za Kuboresha ufunzaji matamshi ya Kiswahili

Baada ya kuwasaili walimu wa Kiswahili, walipendekeza mambo yafuatayo kama mbinu za kuboresha ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Walimu walipendekeza silabasi ya Kiswahili kidato cha kwanza kutoanza na mada za sauti (asilimia 18.37). Vipindi vya Kiswahili kuongezwa (asilimia 14.29), kuwe na maabara ya kufundisha matamshi bora, kuwe na vifaa vya kufunzia kama vile vinasa sauti (24.49), utafiti wa kina katika mada ya matamshi ya Kiswahili kufanywa (asilimia 10.20) na kuwapa wanafunzi mazoezi mengi na ya kutosha.

### 4.2.0 Hojaji kwa Wanafunzi

Hojaji hii ilitusaidia kuzoa habari muhimu za uchunguzi wa data kuhusu changamoto wanazokumbana nazo katika ujifunzaji wao wa matamshi ya Kiswahili kama ifuatavyo;

### 4.2.1 Ni lini mara ya kwanza ulikabiliana na sauti za Kiswahili

Utafiti huu ulilenga kubaini ni lini mara ya kwanza mhojiwa alikabiliana na sauti za Kiswahili. Matokeo ya kipengele hiki cha hojaji yamewasilishwa kupitia jedwali hili.

**Jedwali 12: Ni lini mara ya kwanza ulikabiliana na sauti za Kiswahili?**

| | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kabla ya shule ya msingi | 25 | 29.76 |
| Katika shule ya msingi | 42 | 50.0 |
| Katika shule ya sekondari | 16 | 19.05 |
| Sina uhakika | 01 | 1.19 |
| Jumla | 84 | 100 |

Hapa tulikusudia kujua wakati wanafunzi wasailiwa walipoanza kukabiliana na somo la matamshi ya Kiswahili. Ilidhihirika kuwa asilimia 29.76 ya wanafunzi wasailiwa walianza kukabiliana na somo la matamshi ya Kiswahili kabla ya shule ya msingi. Asilimia 50 ya wasailiwa ilikabiliana na somo hili la matamshi katika shule za msingi. Ni asilimia 19.05 ya wanafunzi wasailiwa walioanza kukabiliana na mada za matamshi katika shule za sekondari. Mwanafunzi mmoja kati ya wale 84 waliohojiwa alikiri kutokuwa na uhakika ni lini mara yake ya kwanza alikabiliana na sauti za Kiswahili yaani asilimia 1.19. Ilidhihirika kuwa somo la matamshi ya Kiswahili halikuwa geni kwa wanafunzi lakini mwendelezo wa kukoleza umilisi wa mada hizi ulikosa. Hii ilibainika kuwa changamoto kubwa.

### 4.2.2 Mtazamo wa Somo la Sauti za Kiswahili

Swali hili lililenga kubaini mtazamo wa wahojiwa kuhusu somo la sauti za Kiswahili kama ilivyowasilishwa katika Jedwali 13 lifuatalo.

**Jedwali 13: Mtazamo wa Somo la Sauti za Kiswahili**

| | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Nalipenda sana | 16 | 19.05 |
| Nalipenda kiasi | 66 | 78.57 |
| Silipendi | 01 | 0.11 |
| Sina uhakika | 01 | 0.11 |
| Jumla | 84 | 100 |

Matokeo ya Jedwali 13 yalidhihirisha kuwa asilimia 19.05 ya wanafunzi wahojiwa walikubali kuwa walipenda somo la sauti sana. Wanafunzi wengi (asilimia 78.57) walikiri kuwa wanapenda somo la sauti kiasi tu. Asilimia 0.11 walisema hawapendi somo la sauti. Aidha, idadi sawa na hiyo ilikiri haina uhakika iwapo inapenda au haipendi somo la matamshi ya Kiswahili. Tulibaini kuwa, mielekeo ya wanafunzi ni changamoto katika ufunzaji na ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

### 4.2.3 Ugumu wa Somo la Sauti

Lengo la kipengele hiki cha hojaji ni kutathmini mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la sauti za Kiswahili na baadaye kuamua kama mielekeo ya wanafunzi ni changamoto katika ufunzaji na ujifunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili. Matokeo ni kama yafuatayo:

**Jedwali 14: Ugumu wa Somo la Sauti**

| | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Gumu sana | 01 | 0.01 |
| Gumu kiasi | 44 | 52.38 |
| Si gumu | 38 | 45.24 |
| Sina uhakika | 01 | 0.01 |
| Jumla | 84 | 100 |

Kutokana na matokeo katika Jedwali 14, ni mwanafunzi mmoja tu (asilimia 0.01) aliyekubali kuwa somo la sauti ni gumu sana kwake. Wanafunzi wengi (asilimia 52.38) walithibitisha kuwa somo la sauti ni gumu kiasi. Asilimia 45.24 waliona somo la sauti si gumu. Mwanafunzi mmoja, yaani asilimia 0.01, hakuwa na uhakika kama somo la sauti ni gumu sana, gumu kiasi au si gumu kwake.

### 4.2.4 Ni Mara ngapi unafanya Mazoezi yanayohusu Sauti ya Kiswahili

Kusudi la kipengele hiki cha hojaji ni kuchunguza ni mara ngapi wanafunzi wanafanya mazoezi ya matamshi na baadaye kubaini ufanyaji wa mazoezi ni changamoto kwa wanafunzi. Matokeo ni kama yalivyowasilishwa katika Jedwali 15 lifuatalo.

**Jedwali 15: Ni Mara ngapi unafanya Mazoezi yanayohusu Sauti ya Kiswahili**

| | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kila siku | 49 | 58.33 |
| Mara moja  kwa mwezi | 16 | 19.05 |
| Mara moja kwa muhula | 09 | 10.72 |
| Sina uhakika | 10 | 11.90 |
| Jumla | 84 | 100 |

Utafiti huu ulionyesha kuwa asilimia 58.33 wanafanya mazoezi ya sauti kila siku. Asilimia 19.05 wanafanya mazoezi hayo mara moja kwa mwezi. Asilimia 10.72 walidai kufanya mazoezi ya matamshi mara moja tu kwa muhula. Nayo asilimia 11.90 hawakuwa na uhakika wowote walifanya mazoezi ya matamshi mara ngapi. Utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi hawafanyi mazoezi ya matamshi ya Kiswahili. Ilibainika kuwa kutofanya mazoezi ya mara kwa mara ni changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili.

### 4.2.5 Changamoto nyingine katika Kusoma Sauti za Kiswahili

Wanafunzi wasailiwa walikubali kukumbwa na changamoto mbalimbali kama vile kutoelewa mwalimu anapofundisha, kutoelewa jinsi ya kutamka sauti, uoga wa kuuliza maswali, ugumu wa kutofautisha au kupambanua sauti kisifa, athari za lugha ya mama pamoja na lugha ya sheng’. Wengine walidai kuwa hali zao za kimaumbile ni changamoto kwao katika ujifunzaji wa matamshi bora.

### 4.2.6 Jinsi ya kuboresha ujifunzaji wa sauti za Kiswahili

Wanafunzi wasailiwa walipendekeza hatua mbalimbali za kuboresha ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili kama vile kufanya mazoezi ya kutosha, kushiriki katika mijadala na ukariri, kuwa makini mwalimu anapofunza, kuiharamisha lugha duni ya sheng', kutumia vinasa sauti, kutunga nyimbo ili kukumbuka sauti, matumizi ya michoro inayofafanua jinsi ya kutamka sauti, kuwa na kamusi ya sauti na kuwepo na mashairi yanayohusu maneno yenye sauti tatanishi.

### 4.3.0 Zoezi kwa Wanafunzi

Tuliwapa wanafunzi watatu wa kidato cha kwanza na watatu wa kidato cha nne zoezi linalohusiana na vipengele mbalimbali vya kimatamshi ya Kiswahili kama vile sifa bainifu za fonimu za Kiswahii (swali la kwanza, la pili, la nne, la sita na la tisa) sifa arudhi za kifonolojia kama mkazo (swali la tatu) , miundo ya silabi (swali la tano  na la saba)  na kiimbo (swali la nane) uchanganuzi wa zoezi kwa wanafunzi umeelezwa kwa kulinganisha matokeo ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na wale wa kidato cha nne kijedwali.

### 4.3.1 Matokeo ya Zoezi kwa kila Kidato

Matokeo ya zoezi kwa wanafunzi kwa ujumla kutegemea kidato yamewasilishwa kupitia jedwali lifuatalo;

**Jedwali 16: Matokeo ya Zoezi kwa kila Kidato**

| | Alama jumla | Wastani | Daraja modi |
|---|---|---|---|
| Kidato cha kwanza | 15 | 8.0 (53.33%) | 8.0 (53.33%) |
| Kidato cha nne | 15 | 7.4 (49.33%) | 7.0 (46.67%) |

Matokeo ya kijumla ya zoezi hili kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza yalidhihirisha kuwa kwa jumla ya alama zote kumi na tano za zoezi hili wanafunzi wa kidato cha kwanza walipata alama ya wastani ya nane yaani asilimia hamsini na tatu nukta tatu tatu. Nayo daraja modi ikawa alama ya nane pia. Wanafunzi wa kidato cha nne walifanya vibaya kuliko wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa sababu alama ya wastani ya wanafunzi wa kidato cha nne waliofanya zoezi ilikuwa alama saba nukta nane yaani asilimia arobaini na tisa nukta tatu tatu. Daraja modi ilikuwa alama saba.

### 4.3.2 Matokeo ya kila Swali katika Zoezi kwa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza

Baada ya zoezi kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza, matokeo yalichanganuliwa kutegemea kila swali na kuwasilishwa kwa Jedwali 17 hadi Jedwali 25 kama ifuatavyo:

**Jedwali 17: Swali la kwanza (tofauti ya irabu na konsonanti)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 5 | 11.9 |
| 2 | 37 | 88.09 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 18: Swali la pili (sifa za fonimu za irabu)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 21 | 50 |
| 1 | 21 | 50 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 19; Swali la tatu (mkazo/shadda)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 26 | 61.9 |
| 1 | 16 | 38.09 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 20; Swali la nne (sifa za fonimu za konsonti)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 22 | 52.38 |
| 1 | 20 | 47.62 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 21: Swali la tano (kutenga silabi)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 16 | 38.09 |
| 1 | 26 | 61.90 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 22: Swali la sita (sauti tata /f/ na /v/)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 36 | 85.71 |
| 2 | 06 | 14.28 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 23: Swali la Saba (miundo ya silabi)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 38 | 90.48 |
| 1 | 03 | 07.14 |
| 2 | 01 | 02.38 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 24: Swali la nane (kiimbo)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 7 | 16.67 |
| 2 | 35 | 83.33 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 25: Swali la Tisa (sifa bainifu za konsonanti)**

| alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 14 | 33.33 |
| 1 | 09 | 21.43 |
| 2 | 22 | 52.38 |
| 3 | 07 | 16.67 |
| Jumla | 42 | 100 |

### 4.3.3 Matokeo ya kila Swali katika Zoezi kwa Wanafunzi wa Kidato cha Nne

Haya ni matokeo ya kila swali kwa wanafunzi wa kidato cha nne kutokana na zoezi teule lililohusu masuala ya matamshi ya Kiswahili. Matokeo yamewasilishwa kijedwali ifuatavyo:

**Jedwali 26: Swali la kwanza (tofauti ya irabu na konsonanti)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 26 | 38.09 |
| 2 | 16 | 61.9 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 27: Swali la pili (sifa za fonimu za irabu)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 19 | 45.24 |
| 1 | 23 | 54.76 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 28; Swali la tatu (mkazo/shadda)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 26 | 61.9 |
| 1 | 16 | 38.09 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 29; Swali la nne (sifa za fonimu za konsonti)**

| alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 24 | 57.14 |
| 1 | 18 | 42.85 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 30: Swali la tano (kutenga silabi)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 21 | 50 |
| 1 | 21 | 50 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 31: Swali la sita (sauti tata /f/ na /v/)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 29 | 69.05 |
| 2 | 13 | 30.95 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 32: Swali la Saba (miundo ya silabi)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 39 | 92.86 |
| 1 | 0 | 0 |
| 2 | 3 | 7.14 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 33: Swali la nane (kiimbo)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 07 | 16.67 |
| 2 | 35 | 83.33 |
| Jumla | 42 | 100 |

**Jedwali 34: Swali la Tisa (sifa bainifu za konsonanti)**

| Alama | Idadi marudio | Asilimia |
|---|---|---|
| 0 | 5 | 11.9 |
| 1 | 13 | 30.95 |
| 2 | 16 | 38.09 |
| 3 | 08 | 19.05 |
| Jumla | 42 | 100 |

Kama ilivyothibitishwa katika Jedwali 17 hadi Jedwali 34 swali la kwanza lililohusu tofauti ya kijumla kati ya irabu na konsonanti lilijibiwa vyema na wanafunzi wa kidato cha kwanza ikilinganishwa na wale wa kidato cha nne. Wanafunzi asilimia 88.09 walipata tofauti kamili ilhali katika kidato cha nne ni asilimia 61.9 iliyopata tofauti kamili kati ya fonimu za irabu na konsonanti.

Swali la pili lilihusu sifa bainifu za fonimu za irabu. Asilimia 50 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walipambanua vizuri sifa ya irabu husika nayo asilimia 54.76 ya wanafunzi wa kidato cha nne walipambanua vizuri sifa ya irabu.

Katika swali la tatu kuhusu mkazo, wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na wa kidato cha nne walipata matokeo sawa yaani alama 38.09. Waliweza kuweka mkazo katika silabi inayostahili.

Swali la nne lilihusu upambanuzi wa sifa za fonimu za konsonanti. Wanafunzi wa kidato cha kwanza walikuwa na matokeo bora kuliko wale wa kidato cha nne. Asilimia 47.62 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza waliweza kupambanua sifa za konsonanti ipasavyo lakini ni asilimia 42.85 ya wanfunzi wa kidato cha nne iliyoweza kupambanua sifa za kosonanti vizuri.

Swali la tano lilihusu kutenga silabi za Kiswahili. Wanafunzi wa kidato cha kwanza walifanya vyema katika swali hili kuliko wanafunzi wa kidato cha nne. Asilimia 61.90 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walitenga silabi ipasavyo ilhali ni asilima 50 tu ya wanafunzi wa kidato cha nne iliweza kutenga silabi vizuri.

Swali la sita lilihusu maana ya vitate vilivyofanana na fonimu /f/ na /v/. Hata hivyo matokeo katika swali hili yalikuwa ya chini ikilinganishwa na matokeo ya maswali yailiyotangulia. Wanafunzi wa kidato cha nne hapa walifanya vyema kuliko wanafunzi wa kidato cha kwanza. Asilimia 14.28 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walipata swali hili ilhali asilimia 30.95 ya wanafunzi wa kidato cha nne ilipata swali hili.

Swali la saba lililoshughulikia miundo ya silabi changamano (KKKV) lilifanywa vibaya zaidi na wanafunzi wa vidato vyote viwili. Ni mwanafunzi mmoja tu kati ya wale arobaini na wawili wa kidato cha kwanza aliyeonyesha miundo sahihi ya silabi (asilimia 2.38). Ni wanafunzi watatu tu wa kidato cha nne ndio walioweza kujibu swali hili kwa usahihi (asilimia 7.14). Zaidi ya asilimia 90 kwa kila kidato walipata sufuri katika swali hili.

Swali la nane lilihusu kiimbo. Kiwango sawa cha asilimia 83.33 kwa kila kidato kilipata maana halisi ya kiimbo. Swali la mwisho lililenga sifa bainifu za konsonanti. Vidato vyote viwili vilivyohusishwa katika utafiti huu vilidhihirisha kuelewa sifa bainifu za fonimu za konsonanti. Wanafunzi asilimia 52.38 wa kidato cha kwanza waliweza kupambanua sifa bainifu za angalau konsonanti mbili tofauti. Asilimia 38.09 ya wanafunzi wa kidato cha nne ndio waliweza kupambanua angalau sifa bainifu za konsonanti mbili tofauti.

Kutokana na data ya zoezi kwa wanafunzi, changamoto halisi katika kujibu maswali yanayohusu matamshi ya Kiswahili zimedhihirika wazi. Wanafunzi wa kidato cha nne walizoa matokeo mabaya ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza. Hii ni thibitisho kuwa ufunzaji wa matamshi wa Kiswahili hautiliwi uzito katika vidato vya juu na hivyo kukosa umilisi wa kutosha. Aidha, utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi wamekosa umilisi wa vipengele vya kimsingi sana kwa matamshi. Imedhihirika kuwa asilimia 38.09 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hawawezi kueleza tofauti ya irabu na konsonanti.

Tulibaini kuwa vipengele vya sauti hasa vile vya sifa arudhi kama mkazo na silabi vilifanywa vibaya na wanafunzi. Zaidi ya asilimia 60 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha nne hawakuweza kuweka mkazo katika silabi inavyostahili. Vilevile zaidi ya asilimia 90 ya wanafunzi katika vidato vyote viwili hawakuweza kutunga neno lililo na muundo wa silabi changamano ya KKKV. Isitoshe swali la kubainisha maana ya maneno mawili yaliyotokana na sauti tata /f/ na /v/ lilikuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na hata kidato cha nne. Kutokana na utafiti huu, swali la tatu la utafiti liliweza kujibiwa ilivyokusudiwa.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza changamoto zinazohusiana na ufunzaji matamshi kwa wanafunzi wa shule za upili. Uchunguzi huu ulitokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu iliyokusanywa kutoka kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanafunzi wa kidato cha nne katika shule za upili kaunti ya Murang'a Kenya. Data hiyo ilihusu vipengele vitatu maalum, hojaji kwa wanafunzi, hojaji kwa walimu na zoezi kwa wanafunzi. Tumetalii na kufafanua data hiyo. Sura inayofuata ndiyo itakayokuwa ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii inajikita katika kufafanua na kuyatolea maelezo masuala yanayohusu matokeo, ugunduzi na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kwa muhtasari kuhusu utafiti huu. Hali kadhalika sura hii inatoa maelezo ya ugunduzi ulioafikiwa katika utafiti huu pamoja na mapendekezo ya masuala na vipengele muhimu ambavyo vinaweza kuwa kichocheo na changamoto ya tafiti na uchuguzi mwingine zaidi kuhusu taaluma na somo la matamshi ya Kiswahili kwa ujumla miogoni mwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Hii ni kwa sababu somo la matamshi ndilo msingi wa matawi hayo yote mengine ya kisarufi. Baadhi ya changamoto za matamshi zimechangia kudorora kwa matokeo ya Kiswahili kama tawi msingi la sarufi ya Kiswahili.

## 5.1 Muhtasari

Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kutathimini masuala yanayafunzwa katika shule za upili kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili. Tulilenga vile vile kubainisha mbinu za ufunzaji sauti na matamshi katika shule za upili na kuchuguza changamoto katika ufunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili katika shule za upili.

Katika kutekeleza malengo hayo, vitabu vya kiada vilivyogharamiwa na serikali ya Kenya kufunzia Kiswahili katika kila kidato yaani *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwanza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili*

(K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015). vilipitiwa na data kuhusu yanayofunzwa katika shule za upili kuhusu matamshi ya kiswahili kuchanganuliwa kwa uzingativu wa mhimili wa uwili sifa wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. Aidha, sifa pambanuzi za Chomsky na Halle (1968) zilitumiwa kuchanganua data hii na kuainisha sifa bainifu za sauti za Kiswahili.

Nadharia ya utabia ya Skinner (1957) ilitufaa katika kuangazia suala la mbinu na changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Malengo hayo ya utafiti huu yaliafikiwa kwa uchunguzi wa kieneo. Kaunti ya Murang'a ilihusishwa katika utafiti huu. Utafiti huu ulihusisha hojaji kwa walimu na wanafunzi pamoja na zoezi kwa wanafunzi.

Sura ya kwanza imebainisha madhumuni na mkondo mzima ambao kwao utafiti ulifanywa. Sura hii iliangazia usuli, suala, malengo na maswali ya utafiti huu. Sura hii inaangazia misingi ya kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka yake. Misingi ya kinadharia pamoja na mbinu za utafiti vile vile ni kiini kingine cha sura hii ya kwanza. Mbinu za utafiti zilihusisha vile vile mikakati ya uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

Sura ya pili ilishughulikia dhana za fonetiki na fonolojia kwa undani. Dhana hizi kama zilivyofafanuliwa na wanaisimu tafauti tofauti zilikuwa muhimu sana kwetu kwani utafiti wetu ulihusisha vipashio hivi vya kimatamshi na vya kimsingi kabisa katika lugha yoyote ile.

Sura ya tatu ilishughulikia yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kwa kuzingatia silabasi ya Kiswahili na kwa kuzingatia vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa kufunza Kiswahili katika shule za upili kwa kila kidato. Sura hii iliangazia mahitaji ya silabasi ya Kiswahili kuhusu matamshi ya Kiswahili kwa kila kidato yaani kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Aidha mada za matamshi ya Kiswahili katika vitabu vya kiada katika shule za upili nchini Kenya zilibainishwa katika sura hii kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Vitabu teule vilivyohusishwa katika utafiti huu, ni vile vilivyogharamiwa na serikali ya Kenya kufunza Kiswahili katika shule za upili, yaani *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwaza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015).

Ni katika sura hii ambapo lengo la kwanza la utafiti huu la kutathmini yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili katika shule za upili lilishughulikiwa. Uchanganuzi wa data iliyoimbuliwa kutoka wanafunzi watatu wa kidato cha kwanza na watatu wa kidato cha nne pamoja na walimu wao kutoka shule teule katika kaunti ya Murang'a ndio kiini cha sura ya nne. Data hiyo ilihusu hojaji kwa walimu na wanafunzi. Zoezi hili lilihusisha maswali kutoka vipengele vyote viwili vya kifonolojia, yaani fonolojia matamshi na fonolojia arudhi. Data hii ilisaidia kushughulika lengo la pili na la tatu la utafiti huu yaani mbinu na changamoto za ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Mtindo wa uchanganuzi wa tarakimu sayansi za

kijamii wa S.P.S.S. ulitumika. Sehemu ambata inahusu ugunduzi na matokeo yaliyotokana na uchanganuzi huo wa data.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanahusu ugunduzi uliofanywa na mtafiti kutokana na uchaganuzi wa data. Matokeo hayo yameainishwa na kuratibishwa kimaelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Utafiti huu ulilenga kuchunguza yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili, mbinu na changamoto za ufunzaji na ujifunzaji matamshi ya Kiswahili katika shule za upili.

Utafiti huu uligundua kwamba ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika kidato cha kwanza na cha pili umetiliwa maanani. Katika kidato cha kwanza, vipengele vya kifonolojia na hata vya kifonetiki vinafunzwa. Katika fonetiki wanafunzi wanafunzwa namna ya kutamka sauti mbalimbali na mahali sauti zinatamkiwa. Katika fonolojia, wanafunzi wanabainisha sauti za Kiswahili yaani irabu na konsonanti na namna zinatamkwa pamoja na mahali zinatamkiwa. Aidha, sifa arudhi kama vile silabi, mkazo na kiimbo vinaelezwa kinaganaga. Utafiti huu ulibaini kuwa msingi mzuri wa ufunzaji matamshi ya Kiswahili umewekwa na mada zote zinazofunzwa katika kidato hiki cha kwanza zinalenga mhimili wa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. wa uwili sifa.

Katika kidato cha pili ilibainika kuwa kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili, mada za sauti na matamshi ya Kiswahili zilifunzwa chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza pamoja na kusoma kwa sauti. Utafiti wetu uligundua kuwa matamshi

bora yalitiliwa uzito katika kidato hiki. Utamkaji wa sauti tatanishi, silabi tatanishi, maneno tata na kusoma vitanza ndimi kwa sauti kulifunzwa. Hata hivyo, upambanuzi wa sifa za sauti mbalimbali za Kiswahili pamoja na sifa arudhi kama shadda, silabi na kiimbo hazikuendelezwa katika kidato cha pili.

Utafiti huu ulibaini kuwa katika vidato vya juu, yaani kidato cha tatu na cha nne, mada za sauti na matamshi ya Kiswahili hazikutiliwa maanani sana kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili. Katika vidato hivi, ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili umehusishwa katika stadi ya kusoma pekee. Mwanafunzi anahitajika kusoma kwa sauti magazeti, matangazo mbalimbali pamoja na habari za kitaifa na za kimataifa. Msingi wa sifa za sauti za Kiswahili haurejelewi katika vidato vya tatu na vya nne. Masuala ya shadda, silabi na kiimbo haujazungumziwa katika vidato hivi.

Utafiti huu ulipitia vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na kupendekezwa na serikali ya Kenya kufunzia somo la Kiswahili. Lengo la kupitia vitabu hivi lilikuwa kubaini kama yale yaliyopendekezwa na silabasi yanazingatiwa katika uandishi wa vitabu vya kiada. Vitabu vilivyopitiwa ni vinne yaani kimoja kwa kila kidato. Navyo ni *Uhondo wa Kiswahili Kidato cha Kwaza* (Walibora na Wang'endo, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili* (K.L.B, 2018), *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Tatu* (K.L.B, 2018) *na Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne* (Waititu na Ipara, 2015).

Baada ya kupitia vitabu hivi tuligundua kuwa yaliyomo katika vitabu hivi yalioana kabisa na matarajio ya silabasi ya Kiswahili (KIE, 2002) katika ufunzaji wa mada

za matamshi ya Kiswahili isipokuwa katika *Kiswahili Fasaha kidato cha nne* ambacho hatukubaini chochote kinachohusiana na mada za matamshi ya Kiswahili.

*Uhondo wa Kiswahili Kitabu cha Wanafunzi Kidato cha Kwanza* kina mpangilio wa sura ishirini na moja. Mafunzo ya sauti na matamshi yamehusishwa katika sura za kwanza sita kupitia stadi tatu za ufunzaji yaani kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha pamoja na stadi ya kusoma kwa sauti. Katika kidato cha pili, tulibaini kuwa suala la matamshi ya Kiswahili lilishughulikiwa katika sura za kwanza kumi na mbili kwa jumla ya sura zote ishirini na moja chini ya stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Katika kidato cha tatu, ni sura tatu pekee katika jumla ya sura ishirini na mbili zilizohusisha ufunzaji matamshi ya Kiswahili chini ya stadi ya kusoma kwa sauti. Katika kidato cha nne, hatukubaini mada zozote zilizohusiana na matamshi ya Kiswahili.

Utafiti huu basi uligundua kuwa ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili umetiliwa uzito katika vidato vya chini na kupuuzwa katika vidato vya juu. Mazoezi ya kukoleza umilisi wa mada za matamshi katika vidato vya juu haukudhihirika. Tuligundua udhaifu huu kutokana na uchanganuzi wa data yetu ya yanayofunzwa kuhusu matamshi ya Kiswahili kwa mujibu wa kitabu cha *Kiswahili Fasaha kwa Wanafunzi wa Kidato cha Nne* katika kutayarisha watahiniwa na kukuza umilisi wao kuhusu mada za sauti na matamshi ya Kiswahili.

Katika kidato cha kwanza na cha pili, stadi za kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha pamoja na kusoma kwa sauti vilitumika katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine katika vidato vya juu hakuna maendeleo ya mada zilizofunzwa awali. Stadi moja tu yaani ile ya kusoma kwa sauti ndiyo tu ilihusishwa katika vidato vya juu. Ni dhahiri kuwa uzoefu wa kutosha wa mada za matamshi haupo katika silabasi ya Kiswahili kutoka kidato kimoja hadi kiingine. Utafiti huu ulikisia kuwa hii ndiyo sababu ya wanafunzi kukosa ukomavu wa kimatamshi pindi wanavyopanda katika vidato vya juu.

Utafiti huu uligundua kwamba walimu wanaofunza Kiswahili na mada za matamshi ya Kiswahili katika shule za upili ni walimu waliohitimu vizuri kimasomo. Asilimia 77.8 ya walimu waliohojiwa wana shahada ya kwanza. Asilimia 11.1 ya walimu waliosalia wana shahada ya uzamili.

Mbinu za ufunzaji matamshi zilibainika kuwa nyingi. Baadhi ya mbinu tulizongundua zinatumiwa na walimu kufunzia matamshi ni kama: kutamka sauti mbalimbali, kusikiliza na kuzungumza, kusoma vifungu, kutumia michoro, mbinu ya mazoezi ya mara kwa mara yanayohusu sauti na matumizi ya vinasa sauti (sauti za matamshi zilizorekodiwa).

Aidha tulingundua kuwa wanafunzi hutumia mbinu mbalimbali kujifunza sauti na matamshi ya Kiswahili. Mbinu za ukariri, maigizo, imla, kusoma vifungu, mazungumzo, mijadala, masimulizi na michoro na picha ilidhihirika kutumika na zaidi ya asilimia hamsini ya wanafunzi wasailiwa.

Mbinu iliyotumika zaidi na wanafunzi kujifunza matamshi ya Kiswahili ni mbinu ya kusoma vifungu kwa sauti (asilimia 95.24). Hata hivyo tulibaini kuwa mbinu ya matumizi ya chati, vinasa sauti na ile ya jozi mlinganuo funyu ilitumika na wanafunzi wachache.

Tulikisia kuwa mbinu hizi zilikosa kutumika kwa wingi kutokana na ukosefu au uhaba wa vifaa vya kurekodia sauti, chati zenyewe na kalamu za kuchora chati.

Tajriba ya walimu wanaofunza Kiswahili ilibainika kuwa changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Licha ya walimu kuwa wamehitimu vizuri na zaidi ya asilimia 70 kuwa na shahada ya kwanza; wengi wa walimu walibainika kuwa na tajriba fupi. Asilimia ile kubwa (37.05%) wana tajriba kati ya mwaka moja na miaka mitano tu. Hii huenda ikawa changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili sababu ya kukosa uzoefu wa kutosha wa kufunza mada hizi.

Changamoto ya mielekeo hasi ya walimu kuhusu ufunzaji matamshi ya Kiswahili ilibainika. Takriban asilimia hamsini ya walimu walikiri kupenda kiasi tu kufunza sauti za Kiswahili. Asilimia 7.41 ilikubali kutopenda kufunza matamshi ya Kiswahili kabisa.

Aidha walimu walikiri mielekeo ya wanafunzi wao kuhusu mada za matamshi ya Kiswahili ni hasi. Asilimia 22.22 walikubali wanafunzi wao huchukulia somo la matamshi kuwa gumu. Asilimia sawia na hiyo walisema wanafunzi wao wanapenda somo hilo kiasi tu.

Tuligundua kuwa asilimia 50 ya wanafunzi ilikabiliana na sauti za Kiswahili mara ya kwanza katika shule za upili na hata wengine (asilimia 29.76) kukabiliana na sauti za Kiswahili mara ya kwanza kabla shule ya msingi. Ilidhihirika kuwa somo la matamshi ya Kiswahili halikuwa geni kwa wanafunzi lakini mwendelezo wa kukoleza umilisi wa mada hizi ulikosa katika shule za upili kutoka kidato kimoja hadi kingine. Hii ilidhihirika kuwa changamoto kubwa.

Wanafunzi wenyewe kama ilivyokuwa kwa walimu wao walikiri kupenda kiasi tu somo la matamshi ya Kiswahili. Asilimia 78.57 walisema wanapenda somo hili kiasi. Kuhusu ugumu wa somo la matamshi ya Kiswahili asilimia 52.38 ya wanafunzi waliona somo hili kuwa gumu kiasi.

Hii ni ithibati kuwa mielekeo hasi ya walimu na wanafunzi wao ni changamoto katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Utafiti huu uligundua kuwa walimu walikuwa na changamoto tofauti tofauti katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Baadhi ya changamoto hizo ni:

Wanafunzi kuathiriwa na lugha ya kwanza. Walimu walikiri kuwa wanafunzi wote (100%) walikuwa na tatizo la athari ya lugha zao za kwanza. Vile vile ilibainika kuwa asilimia moja ya wanafunzi waliathiriwa na lugha ya sheng’ katika kujifunza matamshi bora ya Kiswahili. Suala la wanafunzi kukosa msingi bora katika madarasa ya chini liligundulia. Asilimia 85.16 ya wanafunzi walibainika kuwa na msingi duni wa mada za sauti na matamshi ya Kiswahili.

Ukosefu wa vifaa vya kufunzia ulibainika kama changamoto ya ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Asilimia 81.48 walikiri ukosefu wa vifaa muhimu kama changamoto kubwa. Tuligundua kuwa kuwepo kwa vipindi vichache katika lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na lugha ya Kingereza ni changamoto pia. Zaidi ya asilimia 70 ya walimu walitoa maoni haya.

Vile vile asilimia 55.56 ya walimu waliona somo la sauti kupangwa kama sura ya kwanza kidato cha kwanza kama changamoto katika ufunzaji sauti na matamshi. Kuna walimu waliokiri kuwa utayarishaji mbaya wa walimu kutoka vyuo vya walimu na vyuo vikuu katika ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili ni changamoto inayolemaza ufunzaji wa mada hizi katika shule za upili (asilimia 40.74)

Suala la uhaba wa vitabu maalum vya kufunzia sauti za Kiswahili lilibainika kama changamoto kwa walimu wachache (asilimia 33.33). Hii ni kutokana na sera ya serikali ya Kenya ya kugharamia vitabu vyote vya kiada katika shule zote za umma nchini Kenya. Pengine waliodai vitabu ni changamoto kwao vitabu vyenyewe vilikuwa vimechelewa kufika shuleni mwao. Ilibainika kuwa hata walimu wenyewe walio na jukumu la kufunza matamshi ya Kiswahili waliathiriwa na lugha zao za kwanza. Asilimia 29.63 walikiri kuathiriwa na lugha zao za kwanza.

Wanafunzi nao walibainika kuwa na changamoto mbalimbali katika ujifunzaji wa matamshi ya Kiswahili. Baadhi ya changamoto hizi ni: kutoelewa mwalimu anapofundisha, kutoelewa kauli za maswali, ugumu wa kutofautisha au kupambanua sauti kisifa, athari za lugha ya mama pamoja na lugha ya sheng'.

Baadhi yao walidai hali zao za kimaumbile zilikuwa changamoto kwao katika ujifunzaji matamshi bora ya Kiswahili.

Kutokana na data ya zoezi kwa wanafunzi, changamoto halisi katika kujibu maswali yanayohusu matamshi ya Kiswahili zimedhihirika wazi. Wanafunzi wa kidato cha nne walizoa matokeo mabaya ikilinganishwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza. Hii ni thibitisho kuwa ufunzaji wa matamshi wa Kiswahili hautiliwi uzito katika vidato vya juu na hivyo kukosa umilisi wa kutosha. Aidha, utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi wamekosa umilisi wa vipengele vya kimsingi sana kwa matamshi. Imedhihirika kuwa asilimia 38.09 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hawawezi kueleza tofauti ya irabu na konsonanti.

Tulibaini kuwa vipengele vya sauti hasa vile vya sifa arudhi kama mkazo na silabi vilifanywa vibaya na wanafunzi. Zaidi ya asilimia 60 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha nne hawakuweza kuweka mkazo katika silabi inavyostahili. Vilevile zaidi ya asilimia 90 ya wanafunzi katika vidato vyote viwili hawakuweza kutunga neno lililo na muundo wa silabi changamano ya KKKV. Isitoshe swali la kubainisha maana ya maneno mawili yaliyotokana na sauti tata /f/ na /v/ lilikuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na hata kidato cha nne.

Utafiti wetu ulibaini kuwa katika data iliyohusu mbinu na changamoto za ufunzaji matamshi, mihimili ya nadharia ya utabia ya Skinner (1957) ilizingatiwa. Wanautabia walisisitiza ufundishaji wa lugha kuzingatia ukariri wa matamshi mazuri. Ufundishaji wa matamshi kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kwanza

kabla ya stadi zingine na mada za matamshi kufundishwa mwanzo na sarufi na miundo yake kufunzwa baadaye. Mihimili hii ya utabia ulidhihirika katika matokeo ya mbinu za ufundishaji sauti na matamshi ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, maswali ya utafiti yaliweza kujibiwa ilivyokusudiwa.

## 5.3 Mapendekezo

Kutokana na ugunduzi kwamba ufundishaji matamshi umetiliwa uzito zaidi katika vidato vya chini na kupuuzwa katika vidato vya juu kwa mujibu wa silabasi ya Kiswahili na vitabu vya kiada vilivyopendekezwa na kuidhinishwa kufunza Kiswahili katika shule za upili, utafiti huu unapendekeza kuwe na marekebisho ya silabasi ya Kiswahili katika mada za matamshi ya Kiswahili. Hata kama uzito wa ufunzaji matamshi utatiliwa mkazo katika vidato vya chini, kuwe na mwendelezo uo huo katika vidato vya juu ili kukoleza umilisi pindi mwanafunzi anavyopanda kutoka kidato kimoja hadi kingine. Utafiti huu unapendekeza stadi za kusikiza na kuzungumza vihusishwe katika ufunzaji matamshi ya Kiswahili katika vidato vya juu kama ilivyo katika vidato vya chini.

Baada ya utafiti huu kupitia vitabu teule vya kiada vilivyoidhinishwa kufunza Kiswahili katika shule za upili, tuligundua kuwa vipengele vingine kama vya kimofolojia na kisintakisia vinafunzwa katika vidato vyote kwa njia ya mjengano. Kwa mfano, mada za aina za maneno zinafunzwa katika kidato cha kwanza kwa kugusia tu, kidato cha pili mada ii hii inafunzwa kwa undani kiasi, kidato cha tatu aina za maneno na mifano yake zinafunzwa, katika kidato cha nne mada hii

inarudiwa kama mazoezi ya yaliyofunzwa awali. Utafiti huu unapendekeza mpangilio kama huu wa mada za matamshi ya Kiswahili katika silabasi na vile vile katika vitabu teule vya kufunzia matamshi ya Kiswahili katika shule za upili.

Kadhalika kitabu teule kinachotumika kufunzia Kiswahili katika kidato cha nne (*Kiswahili Fasaha*) kilibainika kutozingatia silabasi ya sasa katika ufundishaji matamshi ya Kiswahili. Tunapendekeza kitabu hiki kibadilishwe na wakuza mitalaa wateue kitabu kingine kinacholenga silabasi ipasavyo.

Tunapendekeza pawepo na warsha na makongamano ya kitaifa na kimaeneo kuhusu ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Makongamano hayo yahusishe washika dau wote wanaohusika na ufunzaji Kiswahili. Waandishi wa vitabu, walimu, wahadhiri, wanafunzi, wakuza mitalaa na wote wanaohusika katika ufunzaji matamshi na sarufi ya Kiswahili kwa njia moja na nyingine katika shule za sekondari. Katika makongamano hayo wahusika wote wakiwemo watahini wa Baraza la Mitihani la Kitaifa wakubaliane kuhusu mbinu faafu za ufundishaji na utahini wa mada zinazohusiana na sauti na matamshi ya Kiswahili.

Tunapendekeza vile vile kubuniwe mikakati ya kuondoa mielekeo hasi kuhusu matamshi ya Kiswahili miongoni mwa walimu na wanafunzi wa sekondari. Tunaweza kuanzisha mashindano ya kuwasilisha hotuba, mijadala na kufanya mazoezi yanayohusiana na matamshi na mashindano ya vitanza ndimi kutoka ngazi za shule hadi ngazi za kitaifa. Washindi watuzwe ipasavyo na shule zao. Vilevile ni vizuri vipindi vya ufunzaji matamshi viandaliwe katika vyombo vya habari kote

nchini. Hili litawapa wanafunzi hamasa na motisha wa kujifunza matamshi ya Kiswahili.

Aidha, tunapendekeza vipindi vya Kiswahili katika shule za upili visawazishwe na vile vya lugha nyingine kama Kingereza ili kuwapa nafasi wanafunzi kuwa na muda wa kutosha wa kujifunza matamshi ya Kiswahili na sarufi yake kwa jumla.

Kadhalika, tunapendekeza serikali kupitia Wizara ya Elimu na hazina za maeneo bunge kugharamia ununuzi wa vifaa vya kufunzia matamshi ya Kiswahili kama vile vinasa sauti na chati. Hii itawezesha wanafunzi kuelewa vizuri mada za matamshi ya Kiswahili. Vilevile kuwe na maabara ya lugha ya Kiswahili katika shule za upili itakayoshughulikia ufundishaji matamshi ya Kiswahili.

Mihimili ya Nadharia ya Utabia ya ukariri, kufunza matamshi na sauti za Kiswahili kwanza na kutumia stadi za kusikiliza na kuzungumza zizingatiwe katika ufundishaji na ujifunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili. Aidha, mhimili wa nadharia hii hasa ule wa uumbaji kama ulivyozungumziwa upya na Bruner (1996) wa mwalimu kuelekeza wanafunzi na kuwapa mazingira huru na bora ya kuumba maarifa mapya kutokana na maarifa awali kuzingatiwa katika ufundishaji matamshi ya Kiswahili.

Tunapendekeza kuwe na mwongozo wa walimu wa kufundishia sauti na matamshi ya Kiswahili. Wakuza mitalaa wanapaswa kuandaa diwani teule za kutumika katika ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

Ni pendekezo letu pia katika maandalizi ya walimu wa Kiswahili kutoka vyuo vya walimu na vyuo vikuu yahusishe sarufi na fasihi ya Kiswahili pekee bila kuhusisha masomo mengine kama yalivyo maandalizi ya walimu wa Kiingereza. Kwa kufanya hivi kutakuwa na muda wa kutosha wa kuandaa walimu vizuri na kukuza umilisi wao katika vipengele mbalimbali vya sarufi na fasihi ya Kiswahili ikiwemo sauti na matamshi ya Kiswahili.

Mwisho, tunapendekeza tafiti zaidi kufanywa kuhusu jinsi walimu wa Kiswahili wanavyoandaliwa katika vyuo vyetu vikuu vya umma katika kozi za fonetiki na fonolojia ya Kiswahili. Hatua hii itasaidia kukabiliana na tatizo lililoko la uhuria wa walimu wa kimwelekeo na la mbinu tofauti tofauti za kufundishia matamshi shuleni.

### 5.4 Matatizo

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo machache ambayo yalipelekea udharura wa kubuni suluhisho. Nadharia tuliyokuwa tumeilenga tangu mwanzo ilikuwa nadharia zalishi kielelezo cha S.P.E. Nadharia hii ilikuwa faafu katika kuchanganua data ya yanayofunzwa kuhusu sauti na matamshi ya Kiswahili katika shule za upili. Tuligundua kuwa tulihitaji nadharia nyingine ya kushughulikia vipengele vya ufundishaji matamshi yaani vipengele vya mbinu na changamoto za ufunzaji matamshi ya Kiswahili. Hili tuliliziba kwa kujumlisha nadharia ya pili ambayo ni nadhania ya utabia.

Aidha, tulikumbwa na tatizo la kukusanya data. Katika baadhi ya shule tulinyimwa nafasi ya kuwapa wanafunzi na walimu hojaji kwa madai ya kuvuruga programu za shule. Vile vile kuna baadhi ya shule hatukuwapata walimu wote wawili wa Kiswahili na hivyo kulazimika kurudi tena siku nyingine kuchukua data. Jambo hili liliongeza gharama za utafiti wetu.

Mwisho tulikumbwa na tatizo la baadhi ya walimu na wanafunzi waliosailiwa kutoa habari zisizo za kweli katika hojaji. Hii ilitokana na wasiwasi uliowakumba baada ya kugundua kuwa tulilenga habari muhimu kuhusu shughuli zao za masomo. Hili tulitatua kwa kulinganisha na kulingamua vipengele vya hojaji tofauti zenye habari ya ukuruba kuhusu lengo la uchunguzi wetu. Mfano, ikiwa mwalimu alidai wanafunzi wake walipenda sana somo la matamshi, tulichunguza ukweli wake katika hojaji ambata ya wanafunzi iliyokadiria mielekeo na ugumu wa somo la matamshi kwa wanafunzi. Kwa njia hiyo tuliweza kubaini ukweli wa mambo kwa namna ambayo utafiti wetu haukutatizika.

### 5.5 Hitimisho

Sura hii imekuwa kilele cha utafiti wetu. Imesheheni suala la mkondo wa utafiti wetu. Kwayo, tumetoa muhtasari wa utafiti mzima tulioshughulikia. Aidha tumebainisha ugunduzi wa utafiti huu, sehemu ambayo ni muhimu katika kujenga na kuelezea matokeo ya utafiti huu. Vile vile sura hii imetambulisha mapendekezo kadhaa kutokana na utafiti huu. Mengi ya mapendekezo hayo yatafaa waandalizi wa silabasi ya Kiswahili katika shule za upili. Endapo yatatekelezwa

yatawanufaisha wanafunzi wa sekondari hasa katika somo la Kiswahili, walimu, wahadhiri, waandishi wa vitabu, watafiti na wadau wote wa Kiswahili watafaidika kutokana na mapendekezo ya utafiti huu.

## MAREJELEO

Brunner, J. (1996). *The Culture of Education*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Chieni, N. (2001). Language and Society: Kiswahili a National Language or a Social Class Language? *In Kiswahili a tool for development: The multidisciplinary approach,* Shitemi na wengine (wah.) Eldoret: Moi University Press.

Chomsky, N. & Halle, M. (1968). *The Sound Pattern of English*. New York: Harper and Row.

Gatanga Sub-county (2015). Gatanga Sub-county K.C.S.E. Analysis 2015.

Hartman, R. (1972) *Dictionary of Language and Linguistics.* London: Applied Science Publisher.

Hyman, L. (1975). *Phonology: Theory and Analysis*.New York: Holt, Rinehart & Winston.

IPA (1999). *Handbook of the International Phonetic Association*. Cambridge: Cambridge University Press.

Iribe Mwangi, P. (2010). *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound Changes and Words*.Saarbruken: Verlag.

Kawoya, F. na Ryanga, W. (2010). *ECT 313: Mbinu za Lugha na Fasihi (Fasihi Methods).* Kenyatta University: Institute of Open, Distance & E-learning (ODEL).

Kindija A. K. (2012). *Taaluma ya Fonetiki Matamshi*. Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

King'ei, K. na Musau, M. (2002). *Utata wa Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Didaxis Resources and Services.

K.I.E. (2002). *Secondary syllabus volume 1*. Nairobi: K.I.E.

K.L.B. (2018) a. *Kiswahili Kitukuzwe.Kidato cha 2. Kitabu cha Wanafunzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

K.L.B. (2018) b. *Kiswahili Kitukuzwe.Kidato cha 3. Kitabu cha Wanafunzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

K.N.E.C. (2014). *Regulations for the K.C.S.E. Revised Syllabus 2014*. Nairobi: KNEC.

Lass, R. (1984). *Phonology: An introduction to Basic Phonology*.Cambridge. Cambridge University Press.

Massamba, D.P.B. (2010). *Phonological Theory: History and Development*. DSM: KS

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. na Msanjila Y.P. (2004) *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA) Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, P.B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Milroy, L.and Gordon, M. (2003). *Sociolinguistics. Method and Interpretation*. Oxford: Blackwell Publishers.

Ministry of Education, Science and Technology (2002). *Secondary Education Syllabus, Volume one.* Nairobi: Kenya Institute of Education.

Ministry of Education, Science and Technology (2006). *Teachers Handbook.* Nairobi: Kenya Institute of Education.

M.O.E. (2014). *Murang'a County K.C.S.E. 2014 Examination Result Analysis*. Murang'a: Nazarine computers.

Mugenda, O. and Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Analysis*. Nairobi; ACTS Press.

Musau, M. (1993). *Aspects of Interphonology: The study of Kenyan Learners of Swahili*. Unpublished P.H.D. Thesis, Byreuth African Studies.

Musau, P.M. na Chacha, L.M. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundishia Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Njogu, K. na Nganje, D. (2006). *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Otiende, A. (2013). *Athari za kimofonolojia za Kiolusuba katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu kama Lugha ya pili*. Tasnifu ya M.A. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington D.C.: Centre for Applied Linguistics.

Skinner, B.F. (1957). *Verbal Behaviour*. New York, Appleton.

Tarone, E.E. (1987): *Interlanguage of Phonology.The Acquisition of Second Language Sound System*.Rowley, Newbury House 70-100.

Trudgil (1974). *Sociolinguistic. An Introduction*, Volume 10. The University of Califonia: Penguin Publishers.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI

Waititu, F. na Ipara, I. (2015). *Kiswahili Fasaha kidato cha 4*. Nairobi: Oxford University Press.

Walibora, K. na Wang'endo, F. (2018). *Uhondo wa Kiswahili Kitabu cha Wanafunzi Kidato cha 1*. Nairobi: Moran Publishers.

Wolfram, W. and Schilling-Estes, N. (1998). *American English: Dialects and Variation*.Oxford: Blackwell.

## KIAMBATISHO 1: HOJAJI KWA WANAFUNZI

Mimi ni mwanafunzi wa shahada uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninatafiti kuhusu ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kaunti ya Murang'a Kenya. Ninaomba ushirikiano wako katika kujaza hojaji hii. Ujumbe utakaotoa hapa utakuwa wa siri na utatumika kwa lengo la utafiti huu pekee.

*Habari za kibinafsi*

*Maagizo: Soma hojaji kisha ujibu katika nafasi zilizoachwa wazi au upigie mkwaju panapofaa.*

Kidato cha-------------------------- Kaunti ndogo -------------------------

Kategoria ya shule i) Bweni/ kutwa ii) Wavulana/wasichana/mseto

iii) Kiwango cha; kaunti ndogo /kaunti/kieneo/kitaifa

1. Ni lini mara ya kwanza ulikabiliana na sauti za Kiswahili?

A ☐ kabla ya shule ya msingi

B ☐ katika shule ya msingi

C ☐ katika shule ya sekondari

D ☐ sina uhakika

2. Unachukuliaje somo la sauti za Kiswahili?

A Nalipenda sana ☐ B Nalipenda kiasi ☐

C Silipendi ☐ C Sina uhakika ☐

3. Eleza ugumu wa somo la sauti za kiswahili

A ☐ gumu sana B ☐ gumu kiasi

C ☐ si gumu D ☐ sina uhakika

4. Jaza kwa kutia mkwaju. Unatumia mbinu hizi kujifunza sauti za Kiswahili?

| Mbinu | Ndio | La |
|---|---|---|
| Ukariri | | |
| Vinasa sauti | | |
| Maigizo | | |
| Chati | | |
| Imla | | |
| Kuaoma vifungu | | |
| Mazungumzo/majibizano | | |
| Mijadala | | |
| Masimulizi | | |
| Michoro/picha/vibonzo | | |
| Jozi mlinganuo finyu wa sauti | | |

5. Ni mara ngapi unafanya mazoezi yanayohusu sauti za Kiswahili?

A kila siku B ☐ mara moja kila mwezi ☐

C mara moja kwa muhula ☐ ☐

D sina uhakika

6. Toa maelezo ya changamoto unazokumbana nazo katika kusoma sauti za Kiswahili.

…………………………………………………………………………………………

…………………………..………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………..

7. Toa maoni ya kuboresha ujifunzaji wa sauti za Kiswahili.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………………

## KIAMBATISHO 2: ZOEZI KWA WANAFUNZI

Maagizo: jibu maswali yote.

1. Tofautisha irabu na konsonanti. (alama 2)

2. Taja sauti yenye sifa hizi; irabu ya nyuma wastani (alama 1)

3. Weka shadda katika maneno; embe na ndoo (alama 1)

4. Taja sifa mbili za sauti /h/ (alama 1)

5. Tenga silabi katika neno; wanyweshavyo (alama 1)

6. Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya neno fuja na vuja. (Alama2)

7. Tunga maneno mawili yenye muundo wa silabi; KKKV (alama 2)

8. Eleza maana ya kiimbo. (alama 2)

9. Jaza jedwali hili. (alama 3)

| Sauti | Jinsi ya kutamka | Mahali pa kutamkia | Ghuna/sighuna |
|---|---|---|---|
| /gh/ | | Kaakaa laini | |
| /z/ | | | ghuna |
| /l/ | kitambaza | | |

## KIAMBATISHO 3: HOJAJI KWA WALIMU

Mimi ni mwanafunzi wa shahada uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninatafiti kuhusu ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili katika shule za upili kaunti ya Murang'a Kenya.Ninaomba ushirikiano wako katika kujaza hojaji hii. Ujumbe utakaotoa hapa utakuwa wa siri na utatumika kwa lengo la utafiti huu pekee.

*Habari za kibinafsi*

*Maagizo: Soma hojaji kisha ujibu katika nafasi zilizoachwa wazi au upigie mkwaju panapofaa.*

Kaunti ndogo ya -------------------------

Kategoria ya shule i) Bweni/ kutwa    ii) Wavulana/wasichana/mseto

iii) Kiwango cha; kaunti ndogo /kaunti/kieneo/kitaifa

1. Kiwango cha elimu

   a) Uzamili    b) shahada ya kwanza c) stashahada d) nyinginezo

2. Tajiriba ya ufunzaji kimiaka

   a) 1-5    b) 5-10    c) 10-15    d) 20 na zaidi

3. Eleza mwelekeo wako kuhusu ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

   a) Napenda sana    b) napenda kiasi    c) sipendi    d) sina uhakika

4. Je wanafunzi wako wana mwelekeo upi kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa sauti na matamshi ya Kiswahili?

5. Eleza ni mbinu zipi unatumia kufunza mada za matamshi ya Kiswahili?
6. Je changamoto hizi zinaathiri ufunzaji wako wa mada za sauti na matamshi ya Kiswahili?

| Changamoto | Ndio | La |
|---|---|---|
| Wanafunzi kuathiriwa na lugha za kwanza | | |
| Athari za sheng | | |
| Athari za lugha za kigeni | | |
| Mwalimu kuathiriwa kimatamshi na lugha yake ya kwanza | | |
| Ukosefu wa vitabu maalum vinavyohusisha mada za sauti na matamshi ya Kiswahili | | |
| Ukosefu wa vifaa vya kufunzia kama vinasasauti | | |
| Wanafunzi kukosa msingi bora katika madarasa ya chini | | |
| Utayarishaji mbaya wa walimu kutoka vyuo vya walimu na vyuo vikuu | | |
| Vipindi vichache katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuathiri muda wa mazoezi | | |
| Somo la sauti za Kiswahili kupangwa kama sura ya kwanza katika silabasi ya Kiswahili kidato cha kwanza | | |

7. Pendekeza hatua faafu za kuboresha ufunzaji wa matamshi ya Kiswahili.

**KIAMBATISHO 4: RATIBA YA KAZI KUTOKA MEI 2017 HADI MACHI, 2021**

| Nambari | Shughuli | Muda(miezi) | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Maandalizi ya pendekezo la utafiti | 6 | Mei-oktoba 2017 |
| 2 | Kuwasilisha pendekezo | 1 | Novemba 2017 |
| 3 | Marekebisho na kutetea pendekezo | 13 | Disemba 2017 Januari 2019 |
| 4 | Ukusanyaji data | 9 | Februari- Aprili 2019 |
| 5 | Uchanganuzi data | 1 | Mei-Juni 2019 |
| 6 | Marekebisho | 10 | Juni –Aprili 2020 |
| 7 | Ripoti ya utafiti | 1 | Mei 2020 |
| 8 | Marekebisho ya ripoti kutoka mtahini wa ndani | 10 | Juni 2020- Mei 2021 |

## KIAMBATISHO 5: MAKADIRIO YA BAJETI YA UTAFITI

| | Shughuli | kiwango | Gharama jumla(sh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Usafiri wa kukusanya yaliyoandikwa kuhusu mada | Siku thelatini @sh.1000 | 30,000 |
| 2 | Mtandao | Sh 5,000 | 5,000 |
| 3 | Kupiga chapa na kutoa nakala ya pendekezo | Nakala*- sita | 10,000 |
| 4 | Nakala ya vifaa vya utafiti | Nakala 150 | 5,000 |
| 5 | Utafiti mwigo | Siku mbili | 5,000 |
| 6 | Ukusanyaji data | Siku kumi @2,500 | 25,000 |
| 7 | Uchanganuzi data | Sh.10,000 | 10,000 |
| 8 | Nakala ya ripoti ya utafiti | Nakala sita @sh 1500 | 9,000 |
| 9 | Vifaa vya kuandikia | Sh 2,000 | 2,000 |
| 10 | Masurufu | Sh.10,000 | 10,000 |
| | Jumla | | 111,000 |

# KIAMBATISHO 6: IDHINI YA KUKUSANYA DATA YA NYANJANI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/19/58151/29614**

Date: **12th April, 2019**

Harrison Gatuthu Muiga
Kenyatta University
P.O. Box 43844-00100
**NAIROBI.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Tathmini ya ufunzaji matamshi ya kiswahili katika shule za upili Kaunti ya Muranga Kenya"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Murang'a County** for the period ending **12th April, 2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Murang'a County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**


Copy to:

The County Commissioner
Murang'a County.

The County Director of Education
Murang'a County.

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. HARRISON GATUTHU MUIGA***
**of KENYATTA UNIVERSITY, 1539-1000**
**THIKA,has been permitted to conduct**
**research in *Muranga County***

**Permit No : NACOSTI/P/19/58151/29614**
**Date Of Issue : 12th April,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



**on the topic: *TATHMINI YA UFUNZAJI MATAMSHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI KAUNTI YA MURANGA KENYA***

**for the period ending:**
***12th April,2020***

..............................
***Applicant's Signature***

..............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

# KIAMBATISHO 7: SAMPULI YA MAZOEZI YA WANAFUNZI YALIYOSAHIHISHWA

## KIAMBATISHO 3: ZOEZI KWA WANAFUNZI

**Maagizo: jibu maswali yote.**

1. Tofautisha irabu na konsonanti. (alama 2) 0

2. Taja sauti yenye sifa hizi; irabu ya nyuma wastani (alama 1) 0

3. Weka shadda katika maneno; embe na ndoo (alama 1)
e'mbe na nd'oo 0

4. Taja sifa mbili za sauti /h/ (alama 1)
~~hewa hii zuhai~~ hewa hali zuliwi 0

5. Tenga silabi katika neno; wanyweshavyo (alama 1)
wa-nywe-sha-vyo 1

6. Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya neno **fuja na vuja**. (Alama2)
Vuja - ni kuharibu
fuja - ni kunyesha 0


7. Tunga maneno mawili yenye muundo wa silabi; KKKV (alama 2)

8. Eleza maana ya kiimbo.(alama 2)
ni urondaji na ushukaji kwa lugha 0

10. Jaza jedwali hili. (alama 3)

| Sauti | Jinsi ya kutamka | Mahali pa kutamkia | Ghuna/sighuna |
|---|---|---|---|
| /gh/ | | Kaakaa laini | Sighuna ½ |
| /z/ | | | ghuna |
| /l/ | kitambaza | | ghuna 0 |

1½




## KIAMBATISHO 3: ZOEZI KWA WANAFUNZI

**Maagizo: jibu maswali yote.**

1. Tofautisha irabu na konsonanti. (alama 2)
Irabu ni silabi ambazo hazipungi hewa wakati wa matamshi ilhali konsonanti ni silabi ambazo hupunga hewa wakati wa matamshi

2. Taja sauti yenye sifa hizi; irabu ya nyuma wastani (alama 1)
/u/ /o/

3. Weka shadda katika maneno; embe na ndoo (alama 1)
em'be n'doo

4. Taja sifa mbili za sauti /h/ (alama 1)
Hewa hufungiwa pafuni
Haitoi sauti

5. Tenga silabi katika neno; wanyweshavyo (alama 1)
Wa-nywe-sha-vyo

6. Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya neno **fuja na vuja**. (Alama2)
Fuja Vunja sheria Utafuja pekee yako
Vunja vunja sheria pu

7. Tunga maneno mawili yenye muundo wa silabi; KKKV (alama 2)
Kula Kula
Kuza Kuza

8. Eleza maana ya kiimbo.(alama 2)
Kiimbo ni upandishaji na ushushaji wa sauti wakati wa kutamka.

10. Jaza jedwali hili. (alama 3)

| Sauti | Jinsi ya kutamka | Mahali pa kutamkia | Ghuna/sighuna |
|---|---|---|---|
| /gh/ | Kingongo | Kaakaa laini | Si ghuna |
| /z/ | Kikwamizo | meno | ghuna |
| /l/ | kitambaza | ulimi | ghuna |

04

**KIAMBATISHO 8; MAJALADA YA VITABU VYA KIADA VILIVYOIDHINISHWA KUFUNZIA SOMO LA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI KENYA**

